# Uzao Wa Nyoka

Jeffersonville, Indiana, USA
Septemba 28, 1958

1 Mungu mpendwa, Mungu mkuu na mwenye nguvu, aliyeumba vitu vyote kwa nguvu za Roho Wake; na amemleta Yesu Kristo, Mwanawe wa pekee, Ambaye alikufa bure kwa ajili yetu sisi wenye dhambi, Mwenye Haki kwa ajili ya wasio haki, kutupatanisha tena katika ushirika huu wa ajabu tulio nao tena na Mungu. Kama tunavyofundishwa katika Neno lililobarikiwa, ya kwamba tulikuwa na ushirika pamoja Naye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. "Wakati nyota za asubuhi zilipoimba pamoja, na wana wa Mungu walipiga makelele kwa furaha, huko nyuma kabisa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu." Twajuaje kwamba huo haukuwa wakati ule ule ambao Mwana-Kondoo alichinjwa; kwamba hapo Mungu, kwa mawazo Yake matukufu, alituona tukishangilia na kufurahi katika wokovu wetu kwa njia ya Yesu!

Na, usiku wa leo, tuna ladha tu ya ule utukufu mkuu wa Kiungu ambao utafunuliwa katika Kuja Kwake mara ya pili. Magonjwa yote na huzuni vitaondolewa. Ndipo tutakuwa na mwili kama mwili Wake Mwenyewe wenye utukufu, kwa kuwa tutamwona jinsi alivyo. Hapa tunapoiangalia mikono yetu ikichakaa, nywele zetu zikipata mvi, na mabega yakiinama, tunajua ya kwamba sisi ni binadamu na tunaelekea mavumbini ambako vichwa vyetu vimeinamishwa sasa, na tulikotoka. Lakini, Bwana Mungu, hakika tu kama Wewe ulivyo Mungu, ulifanya ahadi ya kwamba tutafufuliwa tena katika siku za mwisho, nasi tunaamini jambo hilo.

2 Kwa uchaji tunasimama pamoja na imani yetu usiku wa leo katika Uwepo Wako, tukija kwa ujasiri kwa sababu Yesu alituagiza kufanya jambo hilo. Si kwa jambo lolote jema tulilofanya, kwa kuwa hatujafanya jambo lo lote lililo sawa; bali tunakuja kwa unyenyekevu, tukikiri kwamba tunamiliki hazina hii kwa sababu ya neema Yake ambayo tumepewa. Kwa hiyo, tunakuja tukiomba ya kwamba utatubariki usiku wa leo katika kulileta Neno. Kwa maana imeandikwa, ya kwamba, "Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu." Na hebu kinywa cha Mungu na kinene usiku wa leo. Jalia maneno yatoke, na nasihi Hilo lizame ndani kabisa ya mioyo yetu sisi, wasikilizaji, nasi tujazwe na Roho Wako na Uwepo Wako. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

3 Le—leo hii na jana, jana usiku, hasa, na leo, tumekuwa tukizungumza juu ya somo, la kwanza, tuliliita, *Kwa Nini Sisi Si Dhehebu.* Nasi tulilifanya zito kwa namna fulani, kwa nini sisi si dhehebu, na ni kwanini sisi hatuamini katika madhehebu. Kwa sababu, tunaona jambo hilo katika Biblia, ya kwamba madhehebu hayakuchaguliwa na Mungu kamwe; iliamriwa na ibilisi; na kulithibitisha kwa Biblia. Na jinsi ambavyo, kwa kupitia madhehebu, kunatokea kosa. Sasa tunasema jambo hili kusahihisha na kuileta maskani hii katika ushirika kwenye Neno la Mungu lililobarikiwa. Kwamba, matumaini yetu hayajajengwa katika yale madhehebu yasemayo, ama yale mtu ye yote asemayo; umejengwa juu ya yale Bwana Mungu amesema. Na hiyo ndiyo njia pekee tunayoweza kusahihishwa vizuri.

4 Na asubuhi hii, nilikuwa na tano, ninaamini, kanuni tano mbalimbali za imani ambazo zimekuja kutokana na madhebehu, ambazo katakata hazijanenwa kabisa katika Biblia, ambazo makanisa ya Kiprotestanti yanazitii, na kufundisha kama fundisho; jambo lile lile ambalo kanisa mama kahaba la Katoliki linahubiri, nayo yametoka yakaingia katika kanisa la Kiprotestanti. Nasi tunatii kitu kile kile ambacho ni kinyume na mahali po pote katika Neno la Mungu.

5 Kanisa la kwanza la kimadhehebu, tulilichunguza alasiri ya leo katika historia ya wazee wa Nikea, wa kanisa la Nikea. Baada ya kifo cha wale mitume, wakaja wazee wa Nikea, nao wakaendelea kwa miaka kadha. Miaka mia tatu na ishirini na mitano, hatimaye ikafika kwenye—huko Nikea, Ufaransa, ambako walikuwa na lile—lile baraza kuu la Nikea. Na kwenye hilo wao wakaanzisha yale mafundisho ya sharti ambayo kanisa Katoliki linayo sasa, na ambayo pia yamepewa Waprotestanti.

6 Na kama nilivyosema katika—katika mafundisho asubuhi ya leo, "Kila moja ya nyakati hizo za kanisa, hadi kufikia ule—kwa ule wakati wa kanisa la Thesalonike, ile miaka elfu moja na mia tano ya nyakati za giza, hakukuwako na wakati hata mmoja ila ule Yeye aliosema,' Mngali mna Jina Langu. '"

Na upande huu mwingine, hawakuwa katika Kristo tena, walitokeza wakiwa na jina la kimadhehebu, "Katoliki, Lutheri, Wesley, Baptisti, Presbiteri, Pentekoste," na kuendelea.

Lakini kabla tu ya mwisho wa wakati, Yeye alisema, "Nimeweka mbele yako mlango uliofunguliwa." Mnaona? Na huo ndio wakati ambao tunaamini tuko ndani yake sasa hivi, wakati wa milango iliyofunguliwa, katikati ya kuondoka kwa mwisho kwa kanisa la Laodikia.

7 Ni miaka mia tatu na ishirini na mitano kabisa kufikia lile baraza la Laodikia. Na hapo wakaigiza taratibu hizi kama vile kunyunyizia, kumwagia, na mabatizo ya uongo, roho mtakatifu wa uongo, mambo haya mengine yote. Waliyaingiza.

Ndipo basi wakati Luther, akiwa kasisi, na akiwa ametoka kwenye kanisa la Katoliki, alileta mambo haya pamoja nalo. Na kutoka hapo akaja Zwingli, kutoka kwa Zwingli akaja Calvin, kutoka kwa Calvin akatokea Wesley, loo, na kuendelea. Nao wanaendelea tu kupokezana mafundisho haya ya sharti. Basi Mungu anawezaje kuliongoza Kanisa Lake, wakati wanafuata barabara ambazo Yeye kamwe hata

hakuwaletea waongozwe katika hizo?

8 Na kumbuka, katika Ufunuo 17, tulimwona "yule mwanamke." Sasa maneno haya ni dhahiri. Yameandikwa katika Biblia, kwa hiyo nadhani ninaweza kuyasema. Ilisema mwanamke huyu alikuwa ni "kahaba." Hiyo ina maana kwamba yeye alikuwa mwanamke mwenye sifa mbaya; ya kwamba alipaswa kuolewa na mume fulani, naye akafanya uasherati na ulimwengu. Naye alikuwa ninii … Alikuwa ni "MAMA WA MAKAHABA," kwa hiyo alikuwa na binti. Nasi tumechora jambo hilo kijiografia ya kwamba, tukiwa katika… Na pale, mimi mwenyewe, nikiliona jambo hilo kwenye Maandiko, nikiona mafundisho yake na kila kitu, ninaamini Bwana ameliweka mstarini kikamilifu, ya kwamba hilo haliwezi kuwa cho chote kingine ila kanisa Katoliki. Hivyo ndivyo tu inavyoweza kuwa. Nalo lilizaa nini? Makanisa ya Kiprotestanti. Kweli kabisa, yeye alifanya hivyo.

Naye alikuwa ameshika kikombe cha mvinyo ya uasherati wake, na alikuwa akiwanywesha wafalme wa dunia. Naye alikuwa ndiye mtawala juu ya dunia yote, tukinena kiroho. Na hiyo ni kweli kabisa. Hakuna lingine …

9 Angalieni, hebu, tungeweza kurudi katika Danieli na tuichukue ile sanamu. Angalieni ile sanamu: kile kichwa cha dhahabu, ule ufalme wa Babiloni; shaba … ama fedha, Wamedi na Waajemi; shaba, Alexander Mkuu, na kadhalika, ule Ufalme wa Kiyunani; kisha dola za Kirumi, Rumi ya Mashariki na ya Magharibi, ile miguu miwili.

Basi angalieni katika falme hizi kumi, ambazo zinakuja hasa na zile pembe kumi ambazo tulikuwa tukizungumza asubuhi hii, katika kila moja ya falme hizo kumi ambazo zilikuwa ziinuke, kulikuweko na chuma na udongo zilizochanganywa pamoja. Na chuma hicho kilitoka kwenye miguu, ambayo ilikuwa Rumi. Na kuna mlia wa Urumi uliochanganywa katika kila taifa lililoko chini ya Mbingu, kupitia kanisa Katoliki. Hiyo ni kweli kabisa. Nao hawangechanganyikana, mahali popote.

10 Nao wangeoana, wenyewe kwa wenyewe. Biblia ilisema wangefanya hivyo. Na waangalie leo. Mvulana wako akiambatana na msichana Mkatoliki; wanapoenda kufunga ndoa, hawana budi kuahidi kuwalea watoto wao wawe Wakatoliki; mnaona, na kadhalika kwa msichana. Mnaona, ni ili kuvunja nguvu za huyo mwingine.

Lakini ni kitu gani? Biblia inadai kitu hicho chote ni kahaba. Sasa utafanya nini? Hiyo ni kweli. Na jinsi dhambi za watu zingepatilizwa… Tulirudi kwenye Kumbukumbu la Torati, kuonyesha ya kwamba mwana haramu, mwana haramu, asingeweza hata kuingia katika kusanyiko la Bwana kwa vizazi kumi na vinne. Hiyo ilikuwa chini ya sheria. Naye Kristo alikuja kuikuza torati. Ni zaidi sana iliyoje leo?

11 Basi kuna nini kwa hawa, imekuwaje kwa maskini wasichana hawa wa kisasa mitaani leo, maskini wanawake hawa wanaovuta sigara, na kuvaa kaptura, wasichana wa kisasa waliokata nywele zao, na kadhalika? Kuna nini? Ni kwa sababu mama yao alifanya hivyo. Ni kupatiliza, maovu, kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Hivyo ndivyo ilivyo. Basi tumepata kitu gani? Tumefikia mahali, si kitu ila ni lundo la uchafu wa dhambi.

12 Hiyo ndiyo sababu Mungu ameiinua Urusi, ng'ambo ile, ikiwa na kombora la atomiki kuliangamiza, kama ilivyokuwa katika siku zilizotangulia ile gharika, wakati Yeye alipoinua mawingu. Hakika, amefanya hivyo. Na Biblia inasema hivyo. Urusi, ingawa ni nchi ya kikafiri, inayokana Mungu, inacheza kabisa kabisa katika mikono ya Mwenyezi Mungu. Kama tu vile Mfalme Nebkadreza alivyokuwa kwa kusudi la kuiangamiza Israeli kwa maana walishindwa kutembea pamoja na Mungu, Urusi inainuka moja kwa moja "kulipizia watakatifu kisasi," kwa kanisa Katoliki, kwa ajili ya damu ya hao watakatifu ambayo limemwaga. Biblia ilisema hivyo. Itaondoa kitu hicho chote.

13 Kwa hiyo angalieni hapa, kama mama yao alikuwa mcheza dansi, na nyanya yao, na mama yao alikuwa malaya, yeye ni nani leo? Mvua nguo stadi wa rumba. Watoto wake watakuwa nini?

Nanyi mnasema, "Hivi Mungu hufanya jambo hilo?" Naam, bwana.

Mungu hupatiliza uovu wa watoto, kizazi, hata vizazi kumi na vinne. Na kama Kristo alikuja kulikuza, tungesema, "Vizazi mia moja, ama vizazi mia tano." Mbona, Yeye alisema, "Watu wa kale, mmewasikia wakisema, watu wa kale, 'Usiue.' Nawaambia, kila amkasirikiaye nduguye, bila sababu, ameua tayari. Mmewasikia wakisema, hao wa kale, 'Usizini.' Bali Mimi nilisema, kila mtu amtazamaye mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini tayari." Yeye aliifanya … Kukuza ni nini? Kuifanya kubwa mara nyingi. Na kama chini ya torati ilikuwa ni vizazi kumi na vinne, itachukua jambo hilo muda gani leo?

14 Na kijana mwanamume, na wanamume wa makamu, na wanaume waliooa hawana heshima tena na nadhiri zao za ndoa. Mbona, wao huwachukua wanawake na kuishi nao mahali po pote, na kama tu mbwa wa kawaida. Mbwa ana heshima bora na uadilifu bora kuliko walionao watu wengine. Nami najua jambo hilo ni zito mno, bali hilo ni kweli.

Kwa nini? Na makanisa yanaendelea moja kwa moja na hayasemi kitu juu yake. Kwa nini? Wanafanya

kama tu mama yao anavyofanya. Makanisa yanarithi jambo hilo. Kwa sababu, kanisa na kanisa hili la Kiprotestanti lilitoka kwenye kanisa Katoliki, zile dhambi za kanisa Katoliki zimepatilizwa juu ya Waprotestanti. Hakika, zimepatilizwa, kwa hiyo chungu hakiwezi kuiita birika kwamba ni "chafu." Ni kweli kabisa.

15 Sasa tunaona, na katika Maandiko, tuliona … Nami sikuona kijikaratasi mezani usiku huu. Nilisema, nioneshe mahali pamoja ambapo Mungu alipata kuyaweka wakfu madhehebu. Nioneshe mahali pamoja ambapo Mungu alipata kumchagua mhubiri mwanamke. Nioneshe mahali pamoja ambapo Mungu alipata kuagiza kunyunyizia. Nioneshe mahali pamoja ambapo Mungu aliwahi kuagiza kumwagia. Nioneshe mahali pamoja ambapo Mungu aliwahi kubatiza mtu yeyote katika jina la 'Baba, Mwana, Roho Mtakatifu.' Tafuta vitu hivyo." Na hata hivyo daima tunayafanya. Yako kabisa tu kanisani.

16 Sasa, nilisema, "Kwa njia yako sababu ya sisi kutokuwa Wabatisti, ni kwa sababu sisi tunaamini katika wao kubatizwa katika Jina la Bwana Yesu Kristo. Hakujawahi kuwa na mtu hata mmoja, katika Biblia, aliyewahi kubatizwa kwa njia nyingine yo yote. Nioneshe mahali pamoja ambapo mtu mmoja alibatizwa katika jina la "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu," nitainua mikono yangu niseme mimi ni nabii wa uongo.

"Na kama Biblia inasema yakupasa 'ubatizwe katika Jina la Yesu Kristo,' hiyo inamaanisha ni lazima ufanye hivyo. Paulo aliwaamuru wabatizwe tena. Haidhuru walikuwa wamebatizwa namna gani, iliwabidi kuja, wakabatizwe tena. Walibatizwa na mtu yule yule aliyembatiza Yesu Kristo; Yohana Mbatizaji. Akasema, 'Huo hautafaa tena. Hamna budi kuja, mkabatizwe tena.' Nao iliwabidi kufanya hivyo kabla hawajampokea Roho Mtakatifu. Ilikuwa ni mpango wa Mungu."

Huenda nikaingia ndani zaidi kidogo kuliko hapo, usiku wa leo. Kwa nini? Yesu hutimiza Neno Lake. Mnaamini jambo hilo? Sasa, karibu ninyi nyote mlikuwa hapa asubuhi ya leo, bali nataka kukaa kidogo zaidi juu ya jambo hilo.

17 Kwa nini Paulo aagi- ... aamrishe jambo hilo baada ya kutekelezwa? Paulo alisema, "Hata Malaika kutoka Mbinguni akija na kuhubiri jambo lingine lo lote, na alaaniwe."

Sasa unasema, "Tuna Nuru mpya juu yake." La, hamna. Hilo ndilo ibilisi alilomletea Hawa, Nuru fulani mpya. Huhitaji Nuru mpya. Unahitaji kutembea katika Nuru ambayo Mungu tayari ameiweka hapa, hivyo tu.

18 Sasa angalia jambo hili, jinsi lilivyo rahisi. Waliposhuka kutoka Mlima wa Kugeuzwa, Yesu aliwaambia, wanafunzi Wake, "Watu husema Mimi Mwana wa Adamu ni nani?"

"Mmoja alisema Wewe 'Ni Musa, ama Eliya, mmoja wa manabii.'"

Akasema, "Ninyi mwasema nini?"

Yeye alisema, Petro alisema, "Wewe ni Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai."

Yeye alisema, "Heri wewe, Simoni, mwana wa Yona; kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia jambo hili." Mnaona, haliji kupitia kwenye seminari. Haliji kupitia kwenye madhehebu. "Mwili na damu havikukufunulia hili. Hukujifunza jambo hilo kupitia shule yoyote ya theolojia. Bali Baba Yangu, aliye Mbinguni, amekufunulia hili. Na juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu; na milango ya kuzimu haiwezi kulishinda," ufunuo wa kiroho wa Yeye ni Nani.

Angalia, "Nami ninasema ya kwamba wewe ndiwe Petro. Nami nitakupa wewe funguo za Ufalme. Na cho chote utakachofunga duniani, nitakifunga Mbinguni; lo lote utakalolifungua duniani, nitalifungua Mbinguni." Sasa, ilimbidi kulitimiza Neno Lake la sivyo hakuwa Mungu. Sasa, na wakati alipofanya jambo hilo, siku chache baadaye; akasulubishwa, akafufuka, akapaa juu Mbinguni, ndipo Petro akaifungua Injili kwenye Siku ya Pentekoste. Alifanya jambo hilo? Yeye, hakika, alifanya hivyo. Sasa angalia, wakati ange …

19 Wote walikuwa wanawadhihaki, kwa sababu walikuwa wamejawa na Roho. Wao waliitwa "wazushi, watakatifu wanaojiviringisha," ama namna fulani ya jina kama hilo. Na hata wao walicheka, wakasema, "Hawa wamelewa kwa mvinyo mpya."

Basi Petro akisimama katikati yao, aliinua sauti yake, akasema, "Waume na ndugu zangu, sikilizeni sauti yangu. Yasikieni maneno yangu, mnisikilize. Watu hawa hawakulewa kama mnavyodhani wamelewa; hii ni saa tatu tu ya asubuhi. Lakini jambo hili ni lile lililonenwa na nabii Yoeli. 'Itakuwa siku za mwisho, ya kwamba nitaimwaga Roho Yangu,' na kile angefanya juu ya wanawe, na binti Zake, na watumishi Wake wanawake, na kadhalika, kwenye siku hiyo."

20 Basi walipoanza kusikia jambo hili, walichomwa mioyoni mwao. Kwa kuwa, walimsikia mtu ambaye hakujua "ABC" zake, hata hivyo iliwabidi kumtambua yeye, kujua alikuwa na kitu Fulani ndani yake, kikimchoma, Roho Mtakatifu. Umkataze? Mbona, ingekuwa ni kama kujaribu kuzima moto, katika jengo

lililokauka, kwenye siku yenye upepo. Usingeweza kufanya hivyo. Yeye alikuwa amejawa na Roho Mtakatifu. Naye alifanya nini sasa?

Wao walisema, "Vema, waume na ndugu zetu, tufanye nini tupate kuokolewa?"

Sasa tahadhari, Petro, una zile funguo za Ufalme. Mnaona?

Sasa, wakati Yesu alipofufuka siku ya tatu, hakuwa na funguo za Ufalme wa Mbinguni. Je! Ulijua jambo hilo? Yeye alisema, "Nina funguo za mauti na kuzimu", bali si za Ufalme, kwa maana zilikuwa zimepewa Petro.

21 Sasa Yeye alisema, "Petro, lo lote utakalolifungua duniani, nitalifungua Mbinguni. Utakalofunga duniani, nitalifunga Mbinguni."

Sasa hapa amesimama na funguo, kuufungulia ulimwengu jambo hili lililobarikiwa. Na hapa ana funguo mkononi mwake. Nao wanauliza, "Tufanye nini tupate kuokolewa?" Sasa, haidhuru yule mtume alisema kitu gani kifanywe, Mungu hana budi kukitambua Mbinguni, iwapo Yeye alimpa mamlaka hayo.

Sasa Petro alisema, "Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina Lake Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu." Hiyo ni kweli? Na hiyo ndiyo sababu huo ufunguo ulifunga mlango Mbinguni dhidi ya jina lingine lo lote, njia nyingine yo yote, utaratibu nyingine—utaratibu mwingine wo wote. Ulifunga duniani, kisha ukafunga Mbinguni, la sivyo Yesu hakutimiza Neno Lake kwa Petro. Na kila mahali katika Biblia walibatizwa, baada ya hapo, walibatizwa katika Jina la Yesu Kristo. Na wale waliobatizwa kabla ya hapo, ilibidi waje na kubatizwa tena, katika Jina la Yesu Kristo, wapate Roho Mtakatifu. Hiyo ni sahihi. Ingali iko vile vile.

22 Kwa hiyo, kama tunafundisha ubatizo katika jina la "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu," ni unabii wa uongo. Sasa sitaki kuwaudhi ninyi, bali sina budi kusisitiza jambo hili ili kwamba kanisa hili lijue ilivyo. Hatuko hapa kama kundi la watu wasio na elimu; tunajua mahali tunaposimama katika Neno la Mungu. Mnaona, tunajua. Ninampa mtu yeyote changamoto anioneshe mahali pamoja ambapo mtu yeyote aliwahi kubatizwa katika jina la "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu." Sasa mtasikiliza unabii wa uongo ama ile Kweli? Yachunguzeni Maandiko. Ni juu yako.

Nioneshe ambapo mtu mmoja katika Biblia, ambapo kanisa lilipata kufanywa madhehebu katika—katika Biblia. Nioneshe katika Biblia ambapo waliwahi kumweka wakfu mwanamke kuwa mhubiri. Nioneshe katika Biblia mahali mambo haya yote, ambayo tumekuwa tukizungumza habari zake, yamepata kuagizwa katika Biblia. Hayamo humo. Niambieni mahali pamoja. Unaenda kwenye dhehebu …

23 Vema, wakati Wamethodisti walipoinuka, walihubiri utakaso. Hilo ni zuri. Lakini, walipofanya jambo hilo, walitengeneza madhehebu, na hilo likatosha. Hiyo ndiyo sababu Biblia ilisema, "Una jina."

Unasema, "Mimi ni Mkristo."

"Vema, wewe ni wa dhehebu gani?"

Unasema, "Mmethodisti," mbona, wewe ni kahaba basi. "Mimi ni Mbatisti," kahaba. "Pentekoste," wewe ni kahaba. Wewe ni mfuasi wa kanisa hilo.

Unapaswa kuwa wa Kristo. Hakuna shughuli na kusema, "Methodisti," "Baptisti." Kama wewe ni Mkristo, wewe ni Mkristo moyoni.

24 Kila moja ya hayo madhehebu yanaweza kuzaa watoto, watoto wa Mungu, hiyo ni kweli. Lakini unapofikiri unaenda Mbinguni kwa sababu tu wewe ni Mmethodisti ama Mbatisti, umekosea. Na hiyo ndiyo sababu tulikaa nje ya kitu hicho.

Kwa nini Wabaptisti hawawezi kuona?

Nilimwuliza Mmethodisti hapa, aliyekuwa anaandika insha, aliandika tu muda mrefu uliopita. Alisema, "Jambo pekee tulilo nalo juu yako, unaambatana sana na Wapentekoste."

Nikasema, "Hivi 'sisi' ni akina nani?"

"Sisi, Wamethodisti."

Nikasema, "Vema, nitakwambia nitakalofanya. Nitakuja jijini mwenu nawe acha Wamethodisti waudhamini." "Loo," kasema, "bila shaka, tusingeweza kufanya hivyo."

Nikasema, "Hivyo ndivyo nilivyowazia. Ninadumu na Wapentekoste kwa sababu Wapentekoste wanaamini jambo hilo. Hiyo ni kweli. Wao wanaliunga mkono. Hao ndio wanaopata faida kwenye jambo hilo."

Ni wangapi waliosoma lile jalada kwenye Gazeti la Life hivi majuzi tu, juu ya kanisa la Kipentekoste?

Ni moja ya jambo kuu sana katika wakati huu. Walipata waongofu wengi sana katika mwaka mmoja kuliko makanisa mengine yote yakiwekwa pamoja. Kwa nini? Hata katika makosa yao, Mungu anawaendeleza, kwa maana waliamini Kweli nao wanapiga hatua mbele pamoja Nayo. Ni Kweli.

25 Lakini tunafanya nini sasa? Mnaona? Hiyo ndiyo sababu sisi si dhehebu. Na kwa hakika tu kama vile Wapentekoste wanavyojiundia madhehebu…

Na wakati huko nyuma kabisa, wakati Roho Mtakatifu alipomwagwa kwanza juu ya kanisa la Kipentekoste, miaka arobaini iliyopita, nao wakaanza kunena kwa lugha, moja ya zile karama. Hiyo ndiyo karama ndogo kuliko zote. Hiyo ndiyo karama iliyo ndogo sana, kulingana na Mtakatifu Paulo, ni kunena kwa lugha. Na mara tu aliposhuka, "Loo," wao walisema, "tunaye sasa," nao wakafanya madhehebu, Baraza Kuu, ambalo sasa ni Assemblies of God. "Loo, hakuna mtu aliye Naye isipokuwa unene kwa lugha," na Mungu akaondoka moja kwa moja kutoka kwao, na akawaacha waketi pale. Hakika. Naam, bwana.

26 Wakaja wale wa Umoja, nao wakapata ubatizo katika Jina la Yesu. Walisema, "Loo, tumempata," wakaunda madhehebu. Wangefanya nini? Mungu alitoka nje moja kwa moja na kuwaacha waketi pale.

Ni kwa ajili ya, "Ye yote atakaye, na aje."

Mnaona, wa Umoja hawawezi kwenda kwa Waassemblies. Waassemblies hawawezi kwenda kwa Waumoja. Nimezungumza na baadhi ya watu bora sana walio nao, Bw. Goss, na Dr. Pope, watu wengi. Watu ambao ni watu mashuhuri katika … Niliketi pamoja nao. Nikasema, "Unawezaje kufundisha ushahidi huo wa kwanza, kama mwanachuoni?"

"Vema," kasema, "Ndugu Branham," mmoja, wawili ama watatu wao, walikuwa waaminifu sana, wakasema, "tunajua jambo hilo ni kosa, lakini tufanyeje? Kama tukisema lo lote kuhusu jambo hilo sasa, mbona, litavuruga mpango mzima." Hakika, nawe hutakuwa askofu tena, ama msimamizi mkuu. Hilo ndilo wazo.

27 Ndugu, afadhali niwe na misheni ndogo pembeni, ama nihubiri chini ya msonobari, na niwe na Kweli, bila shaka, na nijue kwamba unasema Kweli. Mwanadamu anataka Kweli. Nawe unawajibika, kama Mkristo, kutoa ushuhuda wa Kweli. Mungu atakuwajibisha kwa jambo hilo.

Halafu, juu ya mambo haya, kama hujabatizwa katika Jina la Yesu Kristo, na hujafanya mambo haya, na hujampokea Roho Mtakatifu …

Unasema, "Loo, nilinena kwa lugha." Hilo halimaanishi una Roho Mtakatifu.

Nimewaona wachawi, walozi, pepo, na kila kitu kinginecho, wakinena kwa lugha. Hakika. Hawana Roho Mtakatifu, nanyi mnajua jambo hilo. Wanakunywa damu kutoka kwenye fuvu la kichwa cha mwanadamu, na kucheza, na kumwita ibilisi, na kunena kwa lugha. Hakika. Hawana Roho Mtakatifu.

Kwa hiyo, kwa sababu umenena kwa lugha, hiyo haimaanishi umempata. Njia pekee unayojua kwamba unaye, hapo roho yako inaposhuhudia pamoja na Roho Wake, na matunda ya Roho yanakufuata: upendo, imani, furaha, amani, uvumilivu, wema, upole, fadhili. Hapo ndipo unapojua ya kwamba una Roho Mtakatifu. Anajishuhudia Mwenyewe.

28 Sasa, wakati unapojaribu kuridhika, ati kwa sababu wewe ni mfuasi wa Assemblies, ama wa Batisti, ama wa Presbiteri, unaona kile unachofanya? Unachukua jina la kahaba. Hiyo ni kweli kabisa. Ondokeni kwenye kitu hicho. Ondokeni kwake. Simaanishi kutoka kwenye kanisa lako ama cho chote kile; wewe fanya unalotaka juu ya jambo hilo. Bali toka kwenye kutegemea, "Loo, mimi ni Mpresbiteri. Hatuamini katika siku za miujiza." Kwa nini huamini jambo hilo? Biblia inafundisha jambo hilo. "Loo, mimi ni mfuasi wa Kanisa la Kristo. Wanasema siku za miujiza zimepita." Wao ni manabii wa uongo.

Ninaweza kuwaonesha mahali ambapo Yesu Kristo alitoa Nguvu kwa Kanisa, kuponya wagonjwa, na kufufua wafu, na kutoa pepo. Ninampa changamoto mtu yeyote anionyeshe Andiko katika Biblia ambapo aliziondoa Kanisani. Ni kitu gani kilichoziondoa? Fundisho lako la sharti, kweli, si Neno la Mungu. Roho Mtakatifu angali anafanya kazi hiyo, anaendelea vivyo hivyo, Naye atafanya hivyo milele.

Hiyo ndiyo sababu sisi si dhehebu, "Wenye mfano wa utauwa, na wakikana Nguvu zake; watu kama hao ujiepushe nao." Hatuamini katika upuuzi huo.

29 Sasa, ilianzaje? Hatuna budi kuharakisha na kulifikia jambo hilo upesi iwezekanavyo sasa, jinsi ilivyopata kuanza. Sasa tuna Maandiko mengi yaliyoandikwa hapa juu ya Roho Mtakatifu.

Na jambo jingine, tulitoa changamoto jana usiku, juu ya "ustahimilivu wa watakatifu," si kwa jinsi ile Wabatisti wanavyoamini. La, bwana. Hakika natofautiana na Wabaptisti na wazo lao, la nadharia yao ya Ukalvini. Hakika sikubaliani na Wapresbiteri. Sikubaliani na Wamethodisti juu ya njia yao ya mafundisho ya Kiarmenia. Naam, bwana. Lakini wote wawili wana ukweli, bali huna budi kuwarudisha *Hapa* ambapo ni Kweli. Utokapo kwenda nje huko, unapotea nalo. Hakika.

30 Wabatisti wanaingia, wanawabatiza mtu na mkewe hapa, kuwazamisha majini; na mhubiri anawabatiza, tisa juu ya kumi wanavuta sigara, wanarudi na kusimama kule, na kucheza karata, kamari usiku kucha, harakati za huku na huko, na kufanya magendo; na wanawake wote wakivalia kaptura hapa nje, harakati za huku na huko mitaani, na kukata nywele zao, na—na kuvuta sigara na kuzungumza, na karamu ndogo za anasa, na kufanya mizaha michafu. Nawe unauita huo Ukristo? Nawe unafikiri una usalama wa Milele? Unaenda Jehanamu namna hiyo. Hamngeweza kufurahia Mbinguni kwa njia yo yote. La hasha. Huo si usalama wa Milele.

Lakini wakati mtu anapozaliwa mara ya pili kwa Roho Mtakatifu …

Nanyi Wapentekoste, maana mliruka—ruka, mkanena kwa lugha, mkakimbia huku na huko kwenye marefu ya kanisa, hiyo haimaanishi mna usalama wa Milele. Msitie jambo hilo kamwe kichwani mwenu. La, bwana. Bila shaka haimaanishi hivyo. Kwa kuwa, unajua ya kwamba ninii yako mwenyewe—maisha yako mwenyewe yanakushuhudia, ushuhuda, ya kwamba hauko sawa na Mungu. Hiyo ni kweli. Wewe si sawa. Huo si usalama wa Milele, bado.

31 Lakini nataka kuwaulizeni jambo fulani. Kuna usalama wa Milele? Biblia inasema hivyo. Biblia ilisema ya kwamba majina yetu yaliwekwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla ya ulimwengu kuanza.

Kama nilivyosema asubuhi ya leo, ninasema jambo hilo tena. Yule mtu aliyeuandika ule wimbo, "Kulikuwa na jina jipya lililoandikwa huko Utukufuni usiku huu, na ni langu," wazo lake lilikuwa sawa, bali yeye alikuwa amekosea, Kimaandiko. Jina lako halikuandikwa usiku uliookoka.

Jina lako, kulingana na Biblia, kulingana na Ufunuo 13, 17, na kadhalika, "liliwekwa pale kabla ulimwengu haujaanza; Naye Yesu Kristo aliuawa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu."

32 Mungu angewezaje, Ambaye hana kikomo; Mungu asiye na kikomo angewezaje, akijua mwisho kutoka mwanzo, angewezaje Yeye kupata kuiruhusu dhambi kuja duniani, kama isingekuwa kwa sababu fulani?

Ili kuunga tu mkono sasa baadhi ya mambo ambayo tumesema. Ni kitu gani kilichokuwa cha kwanza, Mwokozi ama mwenye dhambi? [Mtu fulani katika kusanyiko anasema, "Mwokozi." — Mh.] Mwokozi, hakika. Ni nani aliye na nguvu zaidi, Mwokozi au mwenye dhambi? Kama Mwokozi anaweza kuondoa dhambi, Yeye ana nguvu zaidi. Vema, kwa nini aliacha dhambi itendeke kwanza? Kuonesha ya kwamba Yeye alikuwa Mwokozi. Ni yupi aliye na nguvu sana, mponyaji ama ugonjwa? ["Mponya."] Mponyaji. Basi kwa nini aliacha magonjwa yaje? Kuonesha ya kwamba Yeye alikuwa mponyaji. Ninajisikia wa kidini sasa hivi. Naam, bwana. Loo, jamani! Hizo ni sifa Zake.

Hiyo ndiyo sababu Yeye huacha shida ije. Hiyo ndiyo sababu Yeye huruhusu huzuni ije, kuonesha ya kwamba Yeye ni furaha. Hakika, ndivyo ilivyo. Hiyo ndiyo sababu tuna usiku, kuthibitisha kuna mchana. Hiyo ndiyo sababu tuna hasira, kuonesha kuna amani. Hakika, ni pande zote mbili. Loo, Yeye ni wa ajabu.

33 Sasa, ilianzaje? Tutalifikia moja kwa moja, upesi tuwezavyo, kwa hiyo sitawaweka usiku kucha. Sasa, hapana budi kuwe na mwanzo wa mambo yote.

Nami nataka kuwaulizeni jambo fulani. Sasa hii huenda … Unaweka tu hili kwenye mfuko wako wa vesti. Si lazima mweke hili pamoja na chakula cha kawaida. Lakini sikilizeni jambo hili.

Kama wewe ni kiumbe cha Milele, basi kamwe hukuwa na mwanzo, ama kamwe huwezi kuwa na mwisho. Kwa kuwa, *Milele* linatokana na neno "ambacho hakina mwanzo wala mwisho."

Hivi hamkumbuki? Nilisema, asubuhi ya leo, jinsi ambavyo Melkizedeki, wakati alipokutana na Ibrahimu akitoka kuwaua wafalme. Na Biblia ilisema, katika Waebrania 7, ya kwamba—ya kwamba, "Lawi alimtolea Melkizedeki sehemu ya kumi, alipokuwa katika viuno vya baba yake Ibrahimu." Ibrahimu akamzaa Isaka; Isaka akamzaa Yakobo; Yakobo akamzaa Lawi. Huyo alikuwa ni baba, babu, na mzaa babu. Na wakati Lawi alipokuwa katika viuno vya mzaa babu yake, Biblia inamsifu kwa kumpa Melkizedeki zaka. Nena kuhusu Milele! Jamani, jamani! Yeye kamwe hakusema, "Alifanya jambo hilo katika kivuli; kwa uwezekano alifanya jambo hilo." Biblia ilisema, "Alitoa zaka." Amina.

34 Basi, kama sisi tulipitia kwenye mzao wa kweli, wakati Paulo alipohubiri Injili nilikuwako nawe ulikuwako. Tutaingilia jambo hilo, hivi punde tu, moja kwa moja mpaka maskioni mwetu. Angalia, hivyo ndivyo Maandiko yanavyodai, kwetu, hata yalirudi huko nyuma kabisa.

Wazia tu! Lawi; halafu Yakobo, baba yake; halafu Isaka, baba yake; halafu Ibrahimu, baba yake; babu yake. Wakati Lawi alipokuwa katika viuno vya babu yake, alimtolea Melkizedeki zaka.

35 Ninataka kuwaulizeni. Ni nani huyu, Ayubu 27 … 38, wakati aliposema, "Ulikuwa wapi nilipoiweka misingi ya nchi? Wakati nyota za asubuhi zilipoimba pamoja, na wana wa Mungu walipopiga makelele kwa furaha?" Ni akina nani hao wana wa Mungu waliokuwa wakipaza sauti kwa furaha? Yesu aliwaambia, ya kwamba, "Nilikuwa na furaha pamoja nanyi kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu." Sisi si viumbe vya

wakati. Sisi ni viumbe vya Milele.

"Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu. Na wote wanaonijia Mimi, nitawapa Uzima wa Milele, na kumfufua katika siku za mwisho. Hakuna mtu awezaye kuwatoa katika mkono wa Baba Yangu, aliyenipa hao." Utapoteaje?

Mnaona, mnatishika. Mnaogopa. Mtaenda huku na huko. Na huo ndio mmoja wa shuhuda bora sana, ulimwenguni, hujafikia mahali po pote bado. Hiyo ni kweli. Mungu anawezaje kukuokoa kama Yeye …

36 Ni wangapi katika kanisa hili mngeinua mikono yenu, na kuamini ya kwamba Mungu hana kikomo? Mnajua maana ya neno *bila kikomo*? Hilo ni kamilifu kabisa. Bila kikomo, huwezi—huwezi kueleza neno *bila kikomo*.

Uliwahi kuchukua kamera yako na kuitegesha kwenye alama ya pasipo kikomo? Naam, linamaanisha tu tangu hapo na kuendelea. Vema. Hakuna njia ya kuirekebisha tena.

Vema, hivyo ndivyo Mungu alivyo. Yeye hana kikomo. Na iwapo hana kikomo, kusingekuwa na mende, hakuna nzi, hakuna kiroboto, hakuna chawa, hakuna funza, wala kitu cho chote kilichopata kuwa duniani, wala kitakachopata kuwa, ila kile Mungu alichojua kabla ya kufanywa kwa ulimwengu. Hilo hapo wazo la bila kikomo.

37 Vema, basi, Mungu asiye na kikomo anayekuokoa hapa, akijua atakupoteza juma lijalo, ama mwezi ujao, ama mwaka ujao, naam, Yeye anaharibu kusudi lile hasa. Yeye hawezi kukupoteza. "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele wala hataingia Hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Hawezi kufanya jambo hilo. Wala tena wewe…

"Yeye aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi; kwa sababu uzao wa Mungu unakaa ndani yake, wala hawezi kutenda dhambi." Anawezaje kutenda dhambi wakati kuna dhabihu ya dhambi kwa ajili yake?

Ninawezaje kuwa mgonjwa wakati nina afya kamilifu? Ninawezaje kuwa kipofu wakati naweza kuona? Loo, jamani! Ninawezaje kuwa jengoni na nje ya jengo wakati ule ule? Ninawezaje kuwa mlevi na asiyelewa wakati uo huo? Huwezi kufanya jambo hilo.

38 Na wakati unapookoka, uko chini ya Upatanisho, na dhambi zako hazihesabiwi kwako. Je! Daudi hakusema, "Heri mtu ambaye Mungu hatamhesabia dhambi, ama kumwona kwamba yuna dhambi"? Mungu hakihesabii dhambi kiumbe Chake. Hilo ni gumu. Hayo si maziwa ya mtindi. Lakini hiyo ni Biblia. Mungu hatamhesabia dhambi mwenye haki.

"Mungu," kwa neema Yake, kwa kuchagua tangu zamani, "maana hapendi mtu ye yote apotee, bali wote wafikilie toba." Bali akiwa asiye na kikomo, na akijua ni nani angekuja na ni nani asingekuja, Yeye angekusudia tangu awali kila kitu kutenda kazi kulingana na mapenzi Yake. Kama hakufanya hivyo, kwa nini aliruhusu dhambi kwanza? Wakati alipokuwa Mwokozi … Kama kusingalikuwa na mwenye dhambi, Yeye asingekuwa kamwe Mwokozi; hiyo sifa, iliyokuwa ndani Yake, isingetolewa.

39 Yeye alipataje kuwa mponya? Yeye alipataje kuwa mponya? Kwa sababu aliruhusu magonjwa yaje, apate kujionesha Mwenyewe mponyaji. Yeye alikuwa mponyaji. Ungewezaje kuwa … Angewezaje kujulikana? Sifa Zake zingewezaje kufanya kazi? Angewezaje kamwe kuwa mponya, kama hakujakuwako na maradhi? Ilimbidi aruhusu magonjwa.

Si ajabu, Paulo alisema, katika Warumi 8. "Ewe mjinga, ni nani anayeweza kumwambia m—mfinyanzi jambo la kuufanyia; ambaye, wakati udongo ulipoinuka na kusema, 'Kwani kuniumba, wewe, kuniumba hivi?' Je! Yeye hakumwinua Farao kwa kusudi lile lile, apate kuonesha utukufu Wake huko Misri? Yeye humfanya mgumu amtakaye, na kumhesabia haki amtakaye. Si Yeye atakaye, wala yeye apigaye mbio, bali ni Mungu arehemuye."

Kwa hiyo, wewe hukuwa na uhusiano wo wote na jambo hilo. Huna hata jambo moja la kufanya. Kama ni neema, kama ni karama ya bure, hakuna kitu unachoweza kufanya juu yake. Mungu amekupa, na hayo ni mapenzi ya Mungu. Hicho ndicho kitu ambacho Mungu amekuchagulia tangu zamani.

40 Biblia ilisema ya kwamba "tumechaguliwa tangu zamani kuwa wana wa kupewa mamlaka, wana wa Mungu, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu." Basi, wakati Mungu alipomchinja Mwana-Kondoo, katika mawazo Yake Mwenyewe, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, kuthibitisha sifa Zake, alichokuwa Yeye; wakati Mwana-Kondoo alipochinjwa, tulichinjwa pamoja Naye. Wakati Damu ya Mwana-Kondoo iliposhikwa katika nia Yake Mwenyewe, kule nyuma kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, jina langu na majina yenu yaliandikwa kwenye kile Kitabu wakati huo, yote katika mawazo Yake makuu.

41 Yeye hana kikomo. Kama sivyo alivyo, kwa nini akaruhusu jambo hilo? Ni nani aliye na nguvu zaidi ya wote, (nimesema,) Mwokozi ama mwenye dhambi? Ni nani aliye na nguvu zaidi? Basi, ilimbidi aliye na nguvu zaidi amruhusu asiye na nguvu sana, Naye hufanya jambo hilo tu kwa ajili ya utukufu Wake. Wakati alipomfanya Lusifa, Yeye alijua angekuwa ibilisi. Ilimbidi kumwacha aweko kuonesha ya kwamba

Yeye alikuwa Mwokozi, yule Kristo. Ilimbidi kuacha jambo hilo litukie namna hiyo.

Naam, hivi Biblia haisemi, ya kwamba, "Mambo yote hutendeka kwa manufaa ya hao wampendao Mungu"? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Kwa hiyo mnaogopa nini?

Na tuamke na kufanya kazi,
Tujitie moyo katika mzozo wo wote.
Msiwe kama ng'ombe bubu wanaosukumwa, hawana budi waombwe na kubembelezwa!
Na mwe shujaa!

42 Ninapenda jambo hilo. Simameni! Shairi fupi lililokuwa linanisaidia sana nilipokuwa mtoto, linasema kitu kama hiki.

Kulikuwako na Mrumi muungwana,
Katika siku za Mfalme wa Kirumi;
Aliyemsikia mwoga anayelia,
Nyuma ya ngome akisema:
"Loo, ni salama katika msunobari kama huu,
Hakuna mtu anayeweza kuutikisa."
"Loo, la," kasema yule shujaa,
"Nitatafuta njia ama niifanye."

43 Haya basi. Hiyo ni kweli. Kama Biblia hii inafundisha ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele … Halikuwa jambo rahisi nilipotoka kwenye maskani hii siku ile, na kila mtu akiniambia ya kwamba jambo hili lingetukia, na jambo lile lingetukia. "Ungedhaniwa kuwa mshupavu wa dini, utupwe gerezani, na shirika lote la madaktari likupinge." Bali Mungu alisema ufanye hivyo. Biblia ilisema Yeye alikuwa Ndiye. Na sasa moto wa ufufuo unawaka katika kila taifa chini ya Mbingu. Kwa nini? Kabiliana na jambo hilo!

Unafanyaje kazi yako kila siku?
Je! Unaogopa kazi unayopata?
Unaweza kuistahimili kazi iliyo mbele?
Una nia iliyochoka na tupu? (Nakichukia kitu hicho.)
Ama unaistahimili kazi iliyo mbele,
Ama uoga daima unapitia kwenye jambo hilo?
Kama ndivyo ilivyo, kabiliana na jambo jingine utakalopata,
Kwa kufikiria utalifanya.

Dumu nayo. Hakika. Kusudia moyoni mwako, kama Danieli. Dumu pamoja na Mungu.

44 "Haya yote yalitukia wapi? Yalitukiaje? Ni kitu gani kinachowafanya watu wawe hivyo? Kwa nini tuko karibu kabisa kuangamizwa? Ndugu Branham, nieleze. Kitu gani kinakufanya ufikiri ya kwamba kitu hiki chote hakina budi kuangamizwa?" Kiliangamizwa mara moja hapo zamani, (sivyo?) katika yale maangamizi ya gharika. Sasa haya hapa yaja baadhi ya mambo yenye kina. Nasi tutajitayarisha kusoma.

45 Sasa nawataka mfungue pamoja nami sasa, kwenye Kitabu cha Mwanzo, mlango wa 3. Kama mkitaka kujua jambo lo lote, ninaweza kuwaonyesha katika Kitabu hiki cha Mwanzo mahali ambapo kila dini na kila itikadi, na kila kitu tulicho nacho leo hii, kilianza katika Mwanzo. Ni wangapi wanaojua ya kwamba Mwanzo maana yake ni "asili"? Hakika.

Tunaona Kanisa Katoliki pale mwanzo, Babeli, mwanzilishi wake ni Nimrodi; tunaliona katikati ya Biblia, tunaliona mwishoni mwa Biblia; tunaona, wakijaribu kuwaingiza wahubiri wanawake, hapo mwanzoni mwa Biblia, kwa kuabudu sanamu ndogo zilizofanywa kwa mizizi. Ni wangapi waliopata kusoma Babeli Mbili kilichoandikwa na Hislop, ile historia? Vema. Tunaona, katika historia hizi. Walikuwa na mwanamke … Na halafu mnakumbuka, hata Yakobo aliiba miungu ya babaye, na bintiye akaificha chini yake naye akaichukua huko nyikani, jambo ambalo lilitia ile kambi unajisi, baadaye. Vema.

46 Hebu na tusome hapa sasa katika Mwanzo.

> *Basi nyoka alikuwa mwerevu kuliko wanyama wote wa mwitu aliowafanya Bwana Mungu. Akamwambia mwanamke, Ati! hivi ndivyo alivyosema Mungu, Msile matunda ya miti yote ya bustani?*
>
> *… Mwanamke akamwambia nyoka, Matunda ya miti ya bustanini twaweza kula;*
>
> *Lakini matunda ya mti … katikati ya bustani, Mungu amesema, Msiyale, wala msiyaguse, msije mkafa.*
>
> *Nyoka akamwambia mwanamke, Hakika hamtakufa:*
>
> *Kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo,*

*mtafumbuliwa macho, (mnaona, kutafuta Nuru mpya), nanyi mtakuwa kama miungu, mkijua mema na mabaya.*

47 Mnaona jinsi jamaa hawa walivyo siku hizi, wakijaribu kuondoa kwenye Biblia? "Mbona, si ni rahisi tu kumwaga, au kunyunyizia, ama hivi, ama vile?" La, bwana. Mungu aliandika mpango, na huo ndio tunaopaswa kufuata, Huu.

*Mwanamke alipoona ya kuwa ule mti wafaa kwa chakula, wapendeza macho, nao ni mti wa kumfanya … kutamanika kwa maarifa, basi alitwaa katika matunda yake akala, akampa na mumewe, naye akala.*

*Wakafumbuliwa macho yao, wote wawili wakajijua … wa uchi, wakashona majani ya mtini, wakajifanyia wenyewe nguo.*

48 Ningetaka kusimama hapa kwa muda kidogo. Sasa, hapana budi kuwe na mwanzo wa kila kitu. Wewe ulikuwa na mwanzo. Sasa sisi … Hapa ndipo ninapotaka kuweka msingi wa jambo hili lote, sasa, tumezungumza habari zake katika mikutano hii miwili iliyopita, na hadi hapa.

Sasa, asubuhi ya leo tulirudi nyuma na kufanya mchezo wa kuigiza, katika Biblia, kwamba wakati Mungu alipokuwa anaifanya dunia, kwamba alipokuwa akitengeneza gesi; halafu hizo gesi zikawa chokaa, na chumvi, na—na vitu mbalimbali. Alikuwa akiufanya mwili wako. Alikuwa akipanga kujenga, kama vile mjenzi mkuu, kama mkandarasi akiweka vifaa vyake kwa mradi wa ujenzi wa nyumba. Yeye alikuwa akiufanya mwili wako, naye alikuwa ameuweka pale. Yeye alijua sawasawa kabisa, katika nia Yake, kitu ambacho kingefanyika.

Mkono *huu*, Mungu aliufanya huo mkono kabla Yeye … alipokuwa akiufanya ulimwengu; bali, aliifanya roho yangu kabla hakujakuwako na ulimwengu. Sasa, lakini mkono huu na mwili huu, Yeye aliufanya wakati alipoumba ulimwengu, maana mwili huu ulitoka ardhini, nao unarudi ardhini. Mungu aliufanya huo. Yeye alipanga vitu vyote katika ramani Yake kuu na mpango Wake.

49 Sasa, wakati alipoanza kuifanya dunia, Yeye alimfanya mtu, na huyo mtu hakuonekana sawa tu. Sasa tulikuwa na jambo hilo, asubuhi ya leo, tulipitia katika mchezo huo wa kuigiza, jinsi ambavyo Ba—Baba alishuka na kumwangalia Mwanawe, aliyefanywa kwa mfano Wake, na kadhalika. Ndipo akamfanyia mke, msaidizi.

Sasa, kumbukeni, ya kwamba, viumbe vyote vya duniani, Adamu alikuwa amevipa majina.

Alikuwa amewafanya ng'o—ng'ombe, na wanyama, na kila kitu. Na leo, sisi … Wanahistoria na—na wataalamu wengi wa sayansi, wamekuwa wakijaribu, kwa miaka elfu sita, kutafuta kiungo kilichopotea, kwamba ni kwa nini mnyama huyo … Mwanadamu ni kiumbe mnyama. Tunajua jambo hilo, ya kwamba tulifanywa…

50 Na mwanamke ni sehemu tu ya mwanamume, kitu kilichotolewa kwa kingine. Mwanamke hakuwa katika uumbaji wa asili. Mungu alikuwa tayari amemaliza kuumba, kwa miaka na miaka na miaka, hata akamfanya mwanamke kutokana na ubavu uliotoka ubavuni mwa mwanamume. Adamu alikuwa amekwisha kuvipa majina viumbe vyote, kila kitu kingine, bali hakuwa na cha kwake mwenyewe. Kwa hiyo, Yeye akamfanyia msaidizi; akatoa ubavu kutoka ubavuni mwake, akafunga jeraha hilo, kisha akamfanyia msaidizi. Na mtu, katika roho yake, alikuwa mwanamume na mwanamke pia.

Na mwanamke ni sehemu tu ya mwanamume. Na mwanamume anapojitwalia mke, na kama yeye ni mke wake kweli, mke aliyepewa na Mungu, yeye atakuwa tu kama sehemu yake kwake.

Hiyo ndiyo sababu mna vurugu nyingi sana katika ndoa, ni kwa sababu unatoka unaenda na kuona msichana fulani mwenye macho mazuri ya hudhurungi ama macho ya samawati, ama kitu kama hicho, na msichana fulani mwenye umbo zuri, nawe unampenda. Mara ya kwanza anapopata mtoto wake wa kwanza, meno hayo yanatoka, naye anapata makunyanzi na kuzeeka, na ndipo unataka kumfukuza. Na baadhi yenu ninyi wanawake mnampata maskini mvulana mdogo aliyechana nywele zake maridadi sana, huku amezimwagilia nusu kopo la mafuta ya nguruwe ya mamaye, na ni zilizojipindapinda. Nazo zote zitang'oka; ninajua jambo hilo kwa ujuzi. Lakini kitu gani kinatukia? Ni kitu gani? Unanaswa na hilo.

Unapaswa kuomba, kwanza, maana mwanamke ni sehemu yako. Na iwapo umemkumbatia mwanamke kwenye kifua chako, na kumchukua awe mke wako, nawe… Anakuwekea chapa. Tutasema hivi ili mpate kufahamu. Basi mwanamke mwingine ye yote kwenye kifua hicho hatalingana na chapa hiyo. Na Mungu atakuwajibisha kwa jambo hilo. Nanyi kumbukeni tu jambo hilo.

51 Ninyi mnaomchukua mke wa mtu mwingine na … Nilisikia leo kuhusu msichana mdogo hapa mjini, maskini mtoto mdogo. Ninamjua. Na mcheza karata fulani akimnunulia nguo kubwa na nzuri, na kadhalika, na kujaribu kumpata namna hiyo. Panya, angefanya jambo kama hilo, hata hawezi kufikiriwa kuwa ni mwanadamu.

Mwajua, mbwa si duni namna hiyo, na hata hivyo mnamwita mama mbwa "mchafu." Yeye ana uadilifu mwingi kuliko nusu ya wanawake wa Jeffersonville walivyo nao. Nanyi mnamwita nguruwe mama mzee "nguruwe jike," naye si… Yeye ana uadilifu zaidi ya wanawake wa Marekani, wengi wao. Hiyo ni kweli kabisa. Sasa, ninajua hilo halipendezi. Nami niliwaambia ningelielezea kinaganaga, nami nawatakeni mjue jambo hilo. Na hiyo ni kweli. Wote, wanawake siku hizi, hata hawajui maadili ni nini. Kasema, "Haliumizi dhamira yangu." Vema, huna yo yote. Angalia. Naam, bwana. Wakati, unajua lililo jema na baya.

52 Sasa angalia. Mtu huyu, alipoumbwa, Mungu aliitenganisha roho yake. Naye akachukua kipande kutoka kwa mwanamume huyo, ubavuni mwake, na kumfanya mwanamke kwa hicho. Kisha akaitoa roho ya kike, inayopendeza ya huyo mtu, na kumfanya mwanamke kwa hiyo. Naye alimfanya huyo mwanamume, dume, lenye maungo.

Basi unapoona mwa—mwa—mwanamume aliye kidogo… wajua, amejipaka rangi makucha, ama cho chote unachokiita kitu hicho, makucha ya vidole vyake; na, wajua, nne upande mmoja na tano mwingine, na—na nywele zilizochanwa maridadi, kisha anapanua mdomo wake mbele, na upuuzi kama huo; mmoja wa wavulana hawa warembo. Kumbuka tu, dada, ndege huyo ana kasoro fulani. Kuna kasoro. Afadhali umwangalie kwa makini.

53 Tena unapomwona mwanamke mwenye sigara upande mmoja wa mdomo wake, huku amevalia ovaroli, na kusema, "Nitakwambia, ewe jamaa, ni kitu gani!" Ndugu, mwangalie maskini msichana huyo. Kuna kasoro fulani kwake.

Mwanamke, anayepaswa kuwa mwanamke, naye anapaswa kuvaa kama mwanamke. Mungu alipomfanya mwanamume, alimfanya kitu kimoja; na akamfanya mwanamke kitu kingine. Basi Mungu anapomvalisha mwanamume, Yeye alimvalisha kwa njia moja, na mwanamke kitu kingine. Nayo Biblia ilisema, "Ni chukizo kwa mwanamke kuvaa vazi linalompasa mwanamume."

54 Nanyi wanawake, mnaovalia maskini suruali hizi na kadhalika, na kuzivaa huku nje, maskini ninii za kale… Mnaziitaje, kaptula? Wanaziitaje …? Loo, ni upuuzi gani huo wao …? La, la, si kaptura, ni hizo nyingine, hizo zenye miguu mirefu. [Kusanyiko linasema, "Visukuma kwa miguu." — Mh.] Visukuma kwa miguuo, na ovaroli, dangarizi.

*Kaingia, kasema, "Hii ni ya mabibi."*

Nikasema, "La, umekosea. Mabibi hawavai vitu hivyo. Wanawake huenda wakavaa, bali mabibi hawavai." Hiyo ni kweli.

Biblia ilisema, "Ni chukizo kwa mwanamke kuvaa vazi ... na kwa mwanamume kuvaa vazi linalompasa mwanamke."

Na mwanamume anazidi kuwa dondoadume, kila siku, na wanawake wanakuwa wanaume zaidi. Kuna nini? Tutaona katika dakika chache, kwa Biblia. Wanawake si wanawake tena. Simaanishi ninyi wanawake Wakristo. Ninazungumza kuhusu watu wa kawaida. Wao wanataka kutenda kama wanaume; wanataka kukata nywele zao kama wanaume; kuweka mikono yao kwenye kaunta, namna hiyo, na kuimba Mungu Ibariki Marekani, huku sigara inatokeza pembeni mwa vinywa vyao.

55 Hushuka kwenda mitaani, watokee kwa nyuma namna hiyo, na moja kwa moja kwenye barabara kuu. Tulihesabu … Ninataka kuwaambia jambo fulani. Na ninyi madereva wanawake, sikilizeni. Mimi na Billy Paul, katika kampeni hii ya mwisho kila mahali nchini, miezi sita, niliweka hesabu ya idadi ya hatia za barabarani. Na kutoka kwa makosa mia tatu, barabarani, unadhania ni wangapi wao walikuwa ni madreva wanawake? Kulikuwa tu kunakosekana… Kumi na tisa wao walikuwa wanaume. Na mia mbili na themanini au, ninaamini ilikuwa hivyo, mia mbili na themanini na mmoja basi wangekuwa ni madereva wanawake. Madereva wanawake! Sasa, sisemi hakuna madereva wazuri wanawake. Lakini yeye atageuka upande wowote.

Nawe unajaribu tu kumshitaki? Hebu na awe kwa namna fulani ana sura nzuri, amesimama pale, akipandisha hizo nywele juu wakati askari anapokuja. "Mbona," yeye angesema, "hakika, umekosea!" Hatuna sheria.

Walithibitisha jambo hilo juzijuzi kwenye ile kesi ya kodi ambayo ndiyo kwanza niimalize. Hatuna sheria. Kama kuna …

56 Si ajabu kwamba wale wabunge wakuu wa Uingereza walisema, "Demokrasia ilikuwa ni tanga tu bila nanga." Hiyo ni kweli, unasimama kwenye kijisanduku cha sabuni, ukiwashawishi watu wakupigie kura. Demokrasia imeoza, na watawala wa mabavu na wengine wote pia. Kitu hicho chote kimeoza. Hakuna ila kitu kimoja tu kwa Mungu kutenda, ni kukiharibu kitu hicho chote, kama Yeye alivyosema angefanya, na kuanza upya. Sasa angalia jinsi tulivyo karibu na kule Kuja.

57 Sasa wakati mwanamke huyu … Yeye alimfanyia msaidizi, naye alipaswa kuwa msaidizi wake. Na

halafu …

Sasa, hapa, sijawahi kuwa na mhubiri wa kukubaliana na jambo hili bado. Nao wanajaribu kulifanya vingine, lakini hata hivyo haina maana kwangu. Wanajaribu kusema ya kwamba Adamu na Hawa walikula matofaa. Ndugu, kama … Sisemi jambo hili kwa mzaha sasa, bali ninataka kulisema. Kwa kuwa, kama kula matofaa kunawafanya wanawake watambue wao ni uchi, afadhali tuwape matofaa tena. Nanyi mnajua hiyo ni kweli.

Mnajua, kula tofaa, hilo silo walilofanya, likawafanya watambue kwamba walikuwa uchi. Bila shaka, haikuwa hilo. Hapana budi ilikuwa ni kujuana kimwili. Ilipaswa iwe, maana wao walitambua walikuwa uchi walipokula tunda hili lililokatazwa. Hivi mwanamke si mti wa matunda? Wewe si tunda la mama yako? Hilo ndilo tunda lililokatazwa kuliwa.

58 Sasa hapa kuna jambo kuu. Sasa kiwango cha karibu kabisa walichofikia wanasayansi kujua mwanadamu alikuwa nini… Wanachimbua mifupa ya kale, wanachukua mifupa iliyokauka, kisha wanachukua vichwa, na wanachukua mafuvu ya vichwa, na mikono, na mifupa, na kujaribu kuifanya ionekane kama mwanadamu. Nao wanajua ya kwamba kitu kilicho karibu sana walichofikia katika kumpata mwanadamu, kinachomfuata, ni sokwe mtu. Ndiye jamii iliyo karibu sana na binadamu; bali hata hivyo hana uhusiano wo wote na mwanadamu, ndiye wa juu zaidi ya wote.

Uhai ulio wa chini sana uliopo ni chura; ulio wa juu sana ni mwanadamu. Mungu alianzia moja kwa moja kule chini kabisa kisha akaendelea moja kwa moja mpaka juu, mpaka akauleta moja kwa moja ukafikia kwenye mfano Wake. Akauleta kutoka kwa ndege na wanyama, na kuendelea juu, hata akafikia kwenye mfano wa Mungu. Yeye alimfanya mtu katika mfano huo. . Huo ndio ulio wa juu sana Ulio wa chini sana ni kiluwiluwi tu aliyegeuka akawa chura, na kadhalika.

59 Naam, kiungo hiki kilichopotea, ambacho wao hawawezi kukipata. Angalia Maandiko sasa. Ninyi, hamtakubaliana na jambo hili, wengi wenu, bali ninataka … Ninawataka tu mliweke mawazoni. Wala msilichukie. Sikilizeni.

Najua wengi wenu ndiyo kwanza mmekuwa mkimsikiliza Dr. DeHaan. Hakika mimi … Kama mtu wa kawaida yake, na ndugu mzuri wa Kibatisti, nami hakika namfurahia. Yeye ana akili zaidi na bongo, na—naye alisahau mengi kuliko yale niliyowahi kujua; maana yeye ni Daktari wa—wa Theolojia, tena ni daktari wa madawa, tena ni Daktari wa Sayansi. Yeye ni mtu mwerevu. Lakini anasema ya kwamba wale… Wakati wana wa Mungu walipowaona wale binti za watu kuwa ni wazuri; yeye anachukua msimamo wa Josephus, na kusema ya kwamba "wao—wao walijiingiza wenyewe katika miili ya binadamu," na kujitwalia wake. Na kulikuwako na wanefili katika nchi ya Nodi. "Nao wakajitwalia wake na kuishi nao, wakati wana wa Mungu, Malaika walioanguka, walipowachukua na kuwaona binti za wanadamu; na tamaa ya kujuana kimwili ilikuwa jambo lililopendwa sana, na hata hivyo wao wakiwa wenye dhambi kutokana na kuanguka, walijiingiza wenyewe katika miili ya binadamu."

Kama wangefanya jambo hilo, wanaharibu kuponya Kiungu, wanaharibu cho chote kile. Kama ibilisi anaweza kuumba, yeye ni sawa na Mungu. Ibilisi hawezi kuumba. Ninawatakeni mnionyeshe mahali pamoja ambapo Ibilisi anaweza kuumba. Hawezi kuumba. Yeye hupotosha tu kile kilichokwisha kuumbwa. Yeye si muumbaji. Yeye ni mpotoshaji tu.

60 Vema, basi, ni kitu gani kilichotukia? Angalia. Hii hapa tafsiri yangu. Hiki hapa kiungo kilichopotea.

Sasa wao wana sokwe mtu, bali huwezi kuzalisha sokwe mtu na mwanamke na kumzaa mtoto. Huwezi kuzalisha mwanadamu na mnyama ye yote. Hawatachanganyikana. Huwezi kumpa damu, mnyama ye yote.

61 Nilipokuwa Afrika, waliwatendea maskini watu hao weusi kule mabaya sana; mtu fulani akaniambia, kasema, "Wao si kitu ila wanyama."

Nikasema, "Samahani. Wao ni wanadamu tu kama wewe ulivyo, labda kidogo zaidi." Hebu niwaambieni, unapokuwa na msimamo wa namna hiyo, unaelekea kuwa mnyama. Nikasema, "Mtu huyo, hata awe mweusi kama chapeo ya jembe, ama ni wa manjano kama boga, ama kama yeye ni samawati kama indigo, angeweza kuokoa maisha yako kwa kukupa damu. Bali usijitie kamwe damu ya mnyama." Bila shaka, yeye ni mwanadamu.

62 Ati kwa sababu tu ngozi moja ilikuwa nyeusi, na hiyo nyingine ni ya hudhurungi, na nyingine manjano, na nyingine ni nyeupe, hilo halina uhusiano wo wote na jambo hilo. Biblia ilisema, "Mungu kwa damu moja aliwaumba watu wote." Na hiyo ni kweli kabisa. Mahali tulipoishi, pakibadilisha rangi zetu, hapakuwa na uhusiano na jambo hilo. Mungu alifanya kwa mmoja—kwa mtu mmoja mataifa yote, damu moja, mataifa yote namna ile ile.

Wachina; mtu mweusi hawezi kusema sasa, mtu mweusi hawezi kusema sasa, ya kwamba, "Mchina yule, yeye—yeye ni wa manjano, mimi sitakuwa na uhusiano wo wote naye." Yeye ni ndugu yako. Nawe

mzungu huwezi kumwambia mtu wa manjano ama mtu mweusi, ye yote yule, "Sina uhusiano wo wote nawe." Yeye ni ndugu yako. Kweli kabisa.

63 Angalia sasa, hili ndilo lililotukia. Ninaamini, na ninaweza kuliunga mkono kwa Biblia, ya kwamba nyoka ndiye aliyefanya jambo hilo. Nyoka ni yule mtu aliyepotea kati ya sokwe na mwanadamu. Maana, sikilizeni, angalieni jambo hili sasa, ya kwamba nyoka hakuwa kiumbe kinachotambaa. Alikuwa "mwerevu" kuliko wanyama wote wa kondeni.

Naam, nilienda nikachukua kamusi, leo, kutoka kila mahali, kuchunguza neno hili, maana ya neno *mwerevu*. Linamaanisha "kuwa na akili, kuwa mjanja," na, tafsiri nzuri sana ya—ya Kiebrania (kutoka m-a-h-a-h, mahah) linamaanisha "kuwa na maarifa halisi ya kanuni za uhai."

64 Sasa hebu na tuangalie jambo hili kwa dakika moja. Yeye ni mwerevu, mjanja, hata hivyo anaitwa "nyoka." Lakini, kumbukeni, alikuwa ndiye mwerevu sana aliyekuwako, na alifanana zaidi na mwanadamu kuliko kitu cho chote kilichokuweko kondeni; aliyekuwa anafanana sana na mwanadamu. Yeye hakuwa kiumbe kinachotambaa. Ile laana ndiyo iliyomfanya kiumbe kinachotambaa. Naye alikuwa … Biblia ilisema yeye ndiye aliyekuwa na sura nzuri sana kuliko wote.

Wala hata ile laana haikuondoa urembo wake wote; hata sasa rangi nzuri sana za nyoka zinapendeza, na madaha yake na ujanja wake. Hata ile laana haikuyaondoa. Lakini, kumbukeni, Mungu alimwambia ya kwamba miguu yake ingetoka naye angetambaa kwa tumbo lake. Nawe huwezi kuona mfupa mmoja katika nyoka unaofanana na wa binadamu, na hiyo ndiyo sababu sayansi imepotea. Lakini huyo hapo.

65 Mungu alificha jambo hilo kutoka kwenye macho ya wenye akili na werevu, na akaahidi kulifunulia wana wa Mungu, katika siku za mwisho wakati wana wa Mungu watakapodhihirishwa, wakati, "Wana wa Mungu waliofurahi hata kabla ya kuwekwa misingi ya dunia." Wakati ule ufunuo mkuu wa Uungu na kadhalika vingeshushwa katika siku za mwisho, Yeye angedhihirisha mambo haya kupitia wana wa Mungu. Mnajua Maandiko yanafundisha jambo hilo. Na tuko hapa. Hiyo ndiyo sababu Mungu anatufunulia mambo haya. Mungu anawaleta wanawe katika kudhihirishwa. Yeye anaenda na kuvuka vikomo vya maarifa yo yote ya mwanadamu, moja kwa moja hadi kwenye funuo za kiroho, na kuushusha chini. Je! hatukuwa tunafundisha, katika Biblia hii, "Hili ni kwa yeye aliye na hekima"? Si yale amesomea katika seminari fulani; bali kile alichojifunza akiwa magotini mwake mbele za Mungu, na yale yaliyompendeza Mungu kumpa. Wana wa Mungu, wakidhihirishwa!

66 Huyu hapa nyoka, sasa hivi ndivyo alivyokuwa yule nyoka; mimi nitawapa maelezo yangu kumhusu yeye.

Tuna ile…tunashuka, kutoka chura, kuendelea hadi kwa kile kiluwiluwi, na kuendelea chini na kuendelea, na kadhalika na kadhalika, hata hatimaye unafikia kwenye tumbili, kwenye sokwe mtu. Na toka sokwe mtu, sasa tunaruka toka sokwe mtu mpaka kwa mwanadamu, nasi tunashangaa kwa nini.

"Vema," sayansi inasema, "sasa ngojeni! Tunaweza kumzalisha mwanamke kwa tumbili na kwa sokwe, halafu vinginevyo, mwanamume azae kwa sokwe." Haitawezekana. Mzalishe na mnyama mwingine ye yote; haitawezekana. Damu haitachanganyana; chukua damu yako, ni damu tofauti kabisa, kabisa.

67 Kuna damu katikati hapa, nao hawawezi kumpata mnyama huyo. Loo, Haleluya, ninajisikia wa kidini sasa hivi. Angalia. Kwa nini? Mungu aliwaficha wao jambo hilo. Hamna mfupa ndani ya nyoka unaofanana na mfupa wa binadamu. Yeye aliweka jambo hilo mbali sana hata lisingegunduliwa na mtu mwerevu.

Nami nitawaonesha mahali anapotoka mtu huyo mwerevu, a—aliko, hata hivyo. Mnaona, yeye hawezi kuja kupitia jambo hilo.

Halina budi kuja kwa ufunuo, "Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa…" "Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu; na milango ya kuzimu haitalishinda," ufunuo wa kiroho. Hivi—hivi Habili alijuaje kumtoa mwana-kondoo, badala ya Kaini kutoa matunda ya kondeni? Lilifunuliwa kwake kiroho. Huupati kwa seminari. Huupati kupitia madhehebu. Unaupata kutoka Mbinguni.

68 Sasa mwangalie yule nyoka, huyu nyoka aliyekuwa kwanza. Hebu na tuchukue picha yake sasa. Yeye ni jamaa mkubwa mno. Yeye yuko kati ya sokwe na mwanadamu. Na, yule nyoka; ibilisi, Lusifa, alijua ya kwamba hiyo ndiyo damu tu ambayo ingechanganyikana na damu hii ya mwanadamu, mtu pekee angeliweza kushughulika naye. Yeye asingeweza kujishughulisha na sokwe mtu, damu hiyo isingechanganyikana. Asingejishughulisha na vitu tofauti. Asingejishughulisha na kondoo. Asingejishulisha na tofauti. Asingejishughulisha na mnyama ye yote; ilimbidi kujishughulisha na huyu nyoka.

Hebu tumchukue sasa tuone anafanana na nini. Yeye ni mtu mkubwa mno, jitu la zamani za kale sana. Huko ndiko wanakopata mifupa hii mikubwa, nami nitawaonesha jambo hili katika Biblia. Sasa angalia kwa makini. Vema. Mtu huyu mkubwa mno, hebu tuseme yeye—yeye alikuwa na urefu wa futi kumi, mabega makubwa mno; alifanana tu kabisa na mwanadamu. Nayo damu yake; baada ya yeye

kushuka akaja, kulinganisha mnyama mmoja na mwingine. Unaweza kuwazalisha wanyama. Na iliendelea kuwa damu ya hali ya juu, maisha ya hali ya juu, hali ya juu, mpaka yanapanda mpaka kwenye milki ya mwanadamu. Bali kiungo cha mwisho hapa, katikati hapa, kilikatwa kikaondolewa. Ni wangapi wanaojua ya kwamba sayansi haiwezi kupata kile kiungo kichilopotea? Ninyi nyote mnajua jambo hilo. Kwa nini? Huyu hapa, yule nyoka. Huyu hapa, jamaa mkubwa mno.

Ndipo ibilisi anashuka, sasa, anasema, "Ninaweza kuvuvia."

69 Sasa wakati unaanza kuwaangalia wanawake, na kucheza pamoja na wanawake, kumbuka, una upako wa ibilisi (na si mke wako mwenyewe).

Angalia, sasa, ibilisi alishuka na akaingia katika yule nyoka. Kisha akamwona Hawa katika bustani ya Edeni, uchi, naye akazungumza juu ya lile tunda la katikati. Katikati inamaanisha "sehemu ya katikati," na kadhalika; mnaelewa, katika kusanyiko lililochanganyikana. Ndipo akasema, "Naam, ni zuri. Ni zuri kwa macho." Alifanya nini? Akaanza kufanya mapenzi na Hawa, halafu akamjua kimwili, kama mume.

70 Basi mwanamke akaona lilikuwa zuri, kwa hiyo akaondoka akaenda akamwambia mumewe, bali tayari alikuwa ametiwa mimba na Shetani.

Ndipo akamzaa mwanawe wa kwanza, ambaye jina lake lilikuwa ni Kaini, mwana wa Shetani.

"Sasa," mnasema, "huo ni uongo."

Vema, tutaona tu kama ni uongo ama ni kweli. "Nami nitaweka uadui kati ya Uzao wako na uzao wa nyoka." Nini? Uzao wa nyoka! Mwanamke alikuwa na Uzao, naye nyoka alikuwa na uzao. "Huo utakuponda kichwa chako, na wewe utamponda Yeye kisigino." Nako kuponda, hapo, kunamaanisha "kufanya Upatanisho." Basi huo hapo "uzao" wako wa nyoka.

Sasa, angalia, hawa hapa wanatokea watu hawa wawili.

Sasa, huyu nyoka, aliposimama pale, jitu hili kubwa mno likasimama pale, lilikuwa na hatia ya kufanya uzinzi na mke wa Adamu. Dhambi inakaa wapi leo? Kitu gani kinayafanya mambo yawe jinsi yalivyo leo? Sasa, mimi—mimi … Hakika mnaweza kufahamu ninalosema. Basi hivyo ndivyo ilivyokuwa.

Basi alipofanya jambo hilo, Mungu akasema, akaanza kuwaita Hawa na Adamu.

Naye akasema, "Nilikuwa uchi."

Naye akasema, "Ni nani aliyekwambia ulikuwa uchi?"

71 Ndipo wakaanza, kwa mtindo wa kijeshi, kulaumiana. Kasema, "Vema, mwanamke uliyenipa Wewe, alifanya jambo hilo. Ndiye aliyenishawishi."

Ati naye akasema, "Nyoka ndiye aliyenipa tofaa"? Vema, mhubiri, jichunguze.

Mwanamke akasema, "Nyoka alinidanganya." Mnajua maana ya *kudanganya?* Linamaanisha "kunajisi." Naye alinajisiwa. Ibilisi hakumpa tofaa kamwe. "Nyoka amenidanganya."

Na ndipo laana ikaja.

72 Yeye akasema, "Kwa sababu ulimsikiliza nyoka badala ya mumeo, umeuondoa Uhai ulimwenguni. Nawe uta—utazidisha uchungu wako; na kuzaa kwako kutakuwa kwa mumeo," na kadhalika.

"Na kwa kuwa ulimsikiliza mke wako, badala ya Mimi (nimekutoa mavumbini; kiumbe kilicho cha hali ya juu sana), utarudi mavumbini."

"Na, nyoka, kwa kuwa umefanya jambo hilo, miguu yako itatoka. Kwa tumbo lako utakwenda, siku zote za maisha yako. Nawe utachukiwa. Na mavumbi yatakuwa chakula chako." Haya basi. Hicho hapo kiungo kile kilichopotea.

73 Sasa huyu hapa Kaini anakuja. Hebu na tuangalie tabia. Huyu hapa Kaini anakuja. Yeye ni kitu nini? Yeye ni mfanyabiashara mwerevu. Yeye hulima mashamba. Mwerevu, mwenye akili; wa kidini, wa kidini sana; angalia—angalia sifa zake sasa. Nenda tu pamoja nami kwa dakika chache zaidi.

Huyu hapa anakuja. Yeye anajua yeye ni mwadilifu. Anataka kwenda kanisani. Yeye humjengea kanisa, humfanyia sadaka. Analeta madhabahu, na kadhalika. Alijenga madhabahu, akaweka maua yake juu yake. Akaweka shamba, matunda ya kondeni, akamtolea Mungu. Kasema, "Haya basi, Bwana. Ninajua tunakula matofaa, hilo ndilo lililosababisha." Baadhi ya watoto wake wana wazo la namna ile ile. Inaonyesha hilo linatoka wapi. Akaleta matofaa yake, kutoka kondeni, akayaweka pale, kasema, "Haya yatafanya upatanisho."

Mungu alisema, "Haikuwa matofaa."

Lakini, kwa ufunuo wa kiroho, Habili alijua ilikuwa ni damu. Kwa hiyo akamleta mwana-kondoo, akamkata koo, naye akafa.

Ndipo Mungu akasema, "Hiyo ni kweli. Hilo ndilo lililosababisha jambo hilo. Ilikuwa ni damu." Mnajua ni damu gani ninayonena habari zake. Vema. "Damu ndiyo iliyosababisha jambo hilo."

74 Sasa angalia. Na basi Kaini alipomwona ndugu yake mtakatifu anayejiviringisha amekubalika mbele za Mungu, na ishara na maajabu zilikuwa zikitendeka kule, alimwonea wivu. Akasema, "Tutakomesha upuuzi huu sasa hivi." Waangalie ndugu zake, waangalie watoto wake, siku hizi. "Naam, mimi ni mwerevu kuliko alivyo yeye," kwa hiyo akakasirika. Hasira ilitoka wapi? Ungeweza kusema ya kwamba hasira …? Alimwua ndugu yake. Yeye alikuwa muuaji.

Ungeweza kumwita Mungu muuaji? Na Adamu alikuwa mwana wa Mungu. Biblia ilisema, ya kwamba, "Adamu alikuwa mwana wa Mungu," ule mwanzo msafi kule nyuma. Adamu alikuwa mwana wa Mungu. Na ule wivu na husuda, na kila kitu, visingeweza kutoka kwenye mkondo ule msafi.

Ulipaswa kuja kupitia mahali pengine. [Sehemu tupu kwenye kanda — Mh.] Nao ulikuja kupitia kwa Shetani, aliyekuwa mwuaji, kwanza. Biblia ilisema, "Yeye alikuwa mdanganyifu na mwuaji, kwanza." Na ndiyo hilo hapo. Naye akamwua ndugu yake.

Basi huo ulikuwa ni mfano wa mauti ya Kristo. Halafu, kutokana na jambo hilo, bila shaka, Yeye alimwinua Sethi kuchukua mahali pake. Mauti, kuzikwa, na kufufuka kwa Kristo.

75 Angalia, basi, hawa hapa wanefili wako wanakuja. Ndipo Kaini akaenda katika nchi ya Nodi. Kama baba yake alikuwa jitu kubwa mno, Kaini angekuwa kama nani? Baba yake. Naye akaenda kwenye nchi ya Nodi, na kumchukua mmoja wa dada zake.

Njia pekee angeweza kufanya. Hakuna mahali pengine wanawake wangetokea, ila tu kupitia kwa Hawa. Wanadai wao walikuwa na wana na binti sabini. Kama—kama hakukuweko na wanawake… Biblia haiwaandiki wanawake wanapozaliwa, ni wanaume tu. Basi wakati, kama hakukuweko na wanawake wengine ila Hawa, wakati alipokufa, jamii ya binadamu ilikoma kuweko. Ilimbidi kuwa na binti. Na ilimbidi amwoe dada yake mwenyewe.

Alienda katika nchi ya Nodi akampata—akampata mkewe. Basi alipokwisha kumwoa huko, huko ndiko walikowapata wale majitu wakubwa mno, ambao walikuwa ni wana wa Mungu walioanguka; waliokuja kupitia kwa baba yao, ibilisi, kupitia kwa Kaini. Hicho hapo kiungo chako kilichopotea.

76 Na angalia ule uzao wa nyoka. Sasa angalia. Kumbuka, uzao wa nyoka ni wa kidini. Uangalie ukianza kutenda kazi sasa, kwa dakika chache. Huu hapa unaenda, uzao wa nyoka. Ni kitu gani kilichowapata? Sasa hebu nisome tu jambo fulani hapa, nililoandika tu alasiri ya leo.

Ni kitu gani kilichopitia kwenye ukoo wa Habili? Sikilizeni jambo hili. Vema. Moja kwa moja akaja Habili. Baada ya Habili alikuja Sethi. Baada ya Sethi akaja Nuhu. Baada ya Nuhu akaja Shemu. Baada ya Shemu akaja Ibrahimu. Baada ya Ibrahimu akaja Isaka. Baada ya Isaka akaja Yakobo. Baada ya Yakobo akaja Yuda. Baada ya Yuda akaja Daudi. Baada ya Daudi akaja Kristo, kwenye ule ukamilifu.

77 Angalia huko nyuma jinsi Roho wa Mungu alivyoishi katika Habili. Angalia jinsi alivyoishi katika Sethi. Angalia jinsi alivyoishi katika Yuda. Angalia jinsi alivyoishi katika Daudi. Mwangalie Roho yule yule akiita, kupitia ule uzao wenye haki, kote kote kule nyuma. Haidhuru walifanya nini, walikuwa wamechaguliwa tangu asili.

Mwangalie Yakobo, mchafu … Sisemi jambo hili kwa kukufuru. Bali Yakobo, maskini mdanganyifu, akining'inia chini ya koti la mamaye kila wakati; akitangatanga, mvulana dondoadume. Akajivalisha vitu, akaondoka akaenda akamdanganya babaye, kusudi apate zile baraka; bali alipewa hizo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Hakika, alipewa hizo.

Akaondoka akaenda kule akamdanganya baba mkwe wake; na kuchukua vijiti vyenye milia, vijiti vyembamba, kisha akaviweka majini, kuwaogopesha hawa ng'ombe walipokuwa waja wazito; kuwafanya wazae ng'ombe wenye milia, ili apate kudanganya na kuwachukua ng'ombe hao. Mungu alimbariki katika jambo hilo. Hiyo ni kweli.

78 Ole wake mtu ye yote asemaye neno juu ya Yakobo. Mnajua yale—mnajua yale yule nabii wa uongo aliyosema… Ama, alikuwa akitabiri kweli. Balaamu, alisema, "Kila anayembariki atabarikiwa, na kila amlaaniye atalaaniwa."

"Nilikuchukua, Yakobo. Nilimwona kama … kama kwenye nchi ya ugeni. Na kama vile tai avurugavyo kiota chake, nilimvuruga nikamtoa." Haleluya! "Si kwa nguvu, wala uweza, bali kwa Roho Yangu, asema Bwana."

Angalia jambo hilo likifikia ukamilifu huo. Roho huyo alitenda kazi hata kwenye utimilifu katika Kristo,

kupitia kila mmoja wa wale Wazee wetu, akishuka moja kwa moja. Haidhuru walifanya nini, yale waliyosema, yale waliyofanya, walikuwa ni uzao wa wenye haki kabisa.

79 Na, hapa, wakati Ibrahimu mwenye haki … Utukufu! Loo, ninajisikia vizuri sana. Wakati Ibrahimu mwenye haki alipokutana na Melkizedeki, ambaye alikuwa Mungu Mwenyewe!

Melkizedeki alikuwa nani? "Mfalme wa Salemu, ambaye ni Mfalme wa Yerusalemu, Mfalme wa amani. Hakuwa na baba. Hakuwa na mama. Hakuwa na mwanzo wa siku zake, wala mwisho wa uhai wake." Hata awe ni Nani, Yeye yungali hai. "Yeye hakuzaliwa kamwe. Hatakufa kamwe. Kamwe hakuwa na baba wala mama. Hakuwa na mwanzo wa siku zake, wala mwisho wa uhai wake." Niambie Yeye alikuwa nani. Mungu wa milele; katika ule tunaouita ninii…

Loo, ninasahau tu vile mnavyouita huo sasa. Theofani, ndivyo ilivyo. Ni kama tu … Si hadithi ya kubuni; bali hata hivyo ni kitu tu kilichodhihirishwa. Kama vile alivyomjia Ibrahimu hemani kule juu, kama malaika, na kutabiri, na kumwambia Sara alicheka, nyuma Yake, na kadhalika. Kile kitu, kitu kile kile.

Naye alikuwa hapa. Alikutana na Melkizedeki. Na ba-… baba ya babu wa Ibrahimu, katika ule uzao wa wenye haki, akamtolea Melkizedeki zaka; na ilihesabiwa kwa kitukuu chake hapa chini, ule uzao wa wenye haki.

80 Sasa hapa unakuja uzao wa—wa nyoka. Sasa, kumbukeni, kutakuweko na uadui, vita kati yao.

Uzao wa nyoka unakuja, nao unazaa nini? Sasa hebu tuchukue miaka michache ya kwanza. Sasa angalia jambo linalotukia kule. Tutalisoma toka juu, sababu ndiyo kwanza nilichunguze. Uzao wa nyoka ulimzaa Kaini. Kaini akaenda nchi ya Nodi, akazaa wanefili, kisha wakaja kwenye nchi ya Nuhu.

Wao walikuwa watu werevu, wenye elimu, wenye akili. Hiyo ni kweli? Walikuwa wajenzi, wavumbuzi, wanasayansi; si kupitia kwa uzao wa wenye haki, bali kupitia kwa uzao wa Shetani, yule nyoka. Walikuwa watu kama—kama wanasayansi, na wajenzi, na watu mashuhuri, waalimu. Maandiko yanasema hivyo. Walifua shaba. Walifua chuma. Walifua vyuma. Walivumbua vitu. Walifua madini mbalimbali, na wakajenga majumba, na kadhalika. Maandiko yanasema jambo hilo. Nao walikuwa ni wenye kudhihaki Uzao wa mwanamke, Nuhu, mwenye haki. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.]

81 Hebu na tuwafuatilie mbele kidogo. Halafu, tunawafuatilia mpaka kwenye ile safina, kila kitu kiliangamizwa. Ikafikia katika lundo kubwa sana la dhambi, nao wakachukua mamlaka, watu werevu sana na wenye akili sana. Mpaka, Mungu akatazama chini, hawakuwa wamebaki wengi sana, kwa hiyo akamchukua tu Nuhu na jamaa yake akawaingiza katika safina, kisha akanyesha maji akakiangamiza kitu hicho chote. Akamnyakua Henoko, kwanza. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Kulikuwako na uzao wote, karibu uzao wote; bali Yeye ana kusudi halina budi kutimizwa.

82 Basi, Nuhu na wanawe, waliotoka, Ham, Shem, na Yafethi, walitokea kwenye ule uzao wa wenye haki.

Ule uzao ulivukaje? Huo uzao ulikuja kwenye ile safina, kama tu ulivyofanya hapo mwanzo, kupitia kwa mwanamke, wake zao. Wao walibeba uzao wa Shetani, kupitia kwenye ile safina; kama tu vile Hawa alivyobeba uzao wa Shetani, kumzaa Kaini, kwa yule mwanamke.

Mnawaweka hao wanawake katika majukwaa yenu kwa kama wahubiri, Biblia ikilaani jambo hilo! Paulo alisema, "Mtu ye yote akijiona kuwa ni nabii, ama hata kuwa ni wa rohoni, na atambue ya kwamba hayo ninayoandika ni maagizo ya Bwana; bali kama mtu akiwa mjinga, na awe mjinga tu."

83 Hiyo ndiyo sababu nilitoka kwenye kanisa la Kibatisti hapa chini. Ndugu Fleeman alikuwa hapa muda kidogo uliopita; nafikiri alikuwa kule usiku huo. Dr. Davis alisema, "Wewe utasimama hapa ukawaweke wakfu wanawake wawe wahubiri."

Nikasema, "Sitafanya jambo hilo. La, hasha."

Akasema, "Vema, nitakutupa nje."

Nikasema, "Nimefukuzwa kutoka mahali bora zaidi." Nikasema, "Hili ni Neno la Mungu, nalo linalaani kitu hicho. Nami siwezi kushikilia jambo ambalo Mungu amekataa." La, bwana.

Mtu ye yote anayefanya jambo hilo, inaonyesha wao ni waalimu wa uongo, manabii wa uongo. Biblia ilisema wangekuwa. "Wawapoteze walio wateule kama yamkini." Haya basi.

84 Angalia jambo hili sasa. Na kutoka pale, basi, akaja Ham, Ham na mkewe, na hao wengine. Yeye alilaaniwa. Kutoka kwa Ham akaja Nimrod, aliyeujenga Babeli. Kutoka Babeli kulitokea kanisa Katoliki, mwanzo wake. Ukaja kupitia kwa Ahabu. Likashuka kutoka kwa Ahabu, likamwingia Yuda Iskariote; likaishia, kwenye mpinga Kristo.

Na katika siku hizi za mwisho, hii hapa roho ya mpinga Kristo na Roho wa Kristo. Roho ya mpinga-

Kristo, ikisema, "Siku za miujiza zimepita." Roho wa Kristo, akisema, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Roho wa mpinga Kristo akisema, "Haileti tofauti yo yote kama ukibatizwa katika 'Baba, Mwana, Roho Mtakatifu,' ukamwagiwa, ukanyunyiziwa, chochote kile, inamaanisha jambo lile lile." Biblia ilisema ya kwamba Mungu hakosei, wala hawezi kubadilika. Utamtumikia nani? Ni juu yako.

85 Sasa unasema, "Wao wanaweza kuishi pamoja? Ulisema, ya kwamba, mle katika ile safina, Ndugu Branham, kulikuwako na Hamu na Sethi pia." Hiyo ni kweli, kweli kabisa. Hamu alikuwa mwovu. Sethi alikuwa wa kidini na mwenye haki. Vema.

Hebu na tumfuatilie Hamu. Vema, sasa, hao hapo Hamu na Sethi katika safina ile ile; mmoja mwenye haki, na mwingine asiye haki. Kulikuwa na kunguru na hua katika safina ile ile. Kulikuwako na Yuda na Yesu katika kanisa lile lile. Kulikuwako na mpinga-Kristo na Roho Mtakatifu katika kanisa lile lile.

Na, leo, roho zile zile zinafanya kazi. "Wakiwa na mfano wa utauwa, wa kidini sana, bali wakiwa na mfano wa utauwa huku wakikana Nguvu zake; hao nao ujiepushe nao." Roho Mtakatifu, akidai, "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele." Utachagua upande gani?

86 Mpinga-Kristo anasema ya kwamba *Hiki* ni kitabu tu cha kanuni za imani. "Tutakariri Imani ya Mitume." Ninampa changamoto mhubiri ye yote aniambie mahali ambapo Imani ya Mitume inapatikana katika Biblia: "Ninaamini Mungu, Baba Mwenye Nguvu, Muumba wa mbingu na nchi; na Yesu Kristo, Mwanawe. Ninaamini katika Kanisa Takatifu la Katoliki la Kirumi, ushirika wa watakatifu." Unapata wapi jambo hilo katika Biblia? Nanyi mtaikariri katika makanisa yenu makubwa ya Kimethodisti na Kibatisti. Ni fundisho la ibilisi, nao manabii wa uongo wanalifundisha.

87 Nami natumaini siwaudhi, bali ninasisitiza jambo hilo katika maskani hii. Ninyi hapa kwenye Maskani ya Branham, jiepusheni na upuuzi kama huo. Kitu cho chote kinachoamini katika ushirika wa watakatifu ni imani ya mizimu. "Kuna mpatanishi mmoja kati ya Mungu na mwanadamu, na huyo ni Mwanadamu Yesu Kristo." Sijali kuna akina Mariamu wangapi!

Mnaona jinsi uzao huo wa mwanamke kule nyuma ulivyofanya? Mnaona jinsi ule uzao wa mwanamke ulivyopitishwa kule ng'ambo?

Angalieni siku hizi, katika Marekani. Marekani ni uzao wa ibilisi. Ni kitu gani? Ni taifa la mwanamke. Mmesikia, "Huu ni ulimwengu wa wanawake." Hiyo ni kweli. Ni taifa la mwanamke. Ndio wanaoweka mtindo.

88 Nilienda hapa, si muda mrefu uliopita, huko Uswisi. Wanawake wakisema … Maskini mwanamke mmoja aliyejazwa na Roho Mtakatifu akasema, "Unajua, kama nikienda kule Marekani, wao wanasema wanawake wana uhuru."

Nikasema, "Hebu nikwambie jambo hilo linakoelekeza." Nami nikaanza kumwambia.

Akasema, "Loo, rehema, sitaki cho chote cha mambo hayo."

Nikasema, "Huko ndiko jambo hilo linakoongoza."

Mnajua, wao hawafanyi mambo kule kama wanavyofanya hapa.

89 Ni kitu gani? Hebu niwaoneshe ya kwamba Marekani ni mwanamke. Kwenye sarafu yetu kuna picha ya mwanamke. Kila kitu hapa ndani ni mwanamke.

Niambieni, hamna mabaa ya kutosha nchini, ingepasa… Unaweza kuweka mabaa arobaini kwenye jiji hili, na uwaweke malaya watatu, wanawake warembo wanaokatika viuno mitaani; wao watawapeleka watu wengi zaidi jehanamu, wanaowatamani, kuliko mabaa yote ungaliweza kuweka jijini. Hiyo ni kweli kabisa.

Ni nani basi? Ni mwanamke. Yeye ni nini? Yeye ni mungu wa Marekani.

90 Chukua baadhi ya hao maskini wacheza sinema, kisha uje hapa, wameolewa mara nne ama tano, wakiishi na waume watatu ama wanne mbalimbali wakati ule ule; na baadhi ya magazeti haya yakiwaonesha na kuwaambia, yakiwapiga picha wakiwa uchi hapa nje. Nanyi wasichana wadogo mnawaweka hao kama mfano wenu, (kwa nini?) kwa sababu mama yenu aliyewatangulia, labda, nyanya yenu aliyewatangulia. Mnaona mahali huo uzao wa nyoka unapofanya kazi? Hakika, ndivyo ilivyo.

Basi umefanya kitu gani? Kama uovu utapatilizwa kwa vizazi kumi na vinne, chini ya torati, uovu utakuwaje kama ukipatilizwa katika siku hizi, wakati ambapo uzao wa wenye haki uko karibu kwisha? Naye Mungu alisema ungekuja wakati, kama hakuikatiza kazi, kusingesalia na hata mmoja. Tuko katika wakati wa mwisho. Watafute wenye haki usiku wa leo; pita mijini!

91 Loo, unawakuta wafuasi wa kanisa wakiwa waaminifu tu kwa Wabatisti na Wapresbiteri, na kadhalika, kama iwezavyo kuwa. Bali hawana uhusiano wo wote na Mungu zaidi ya sungura asivyo nao

wa kuvaa viatu vya theluji. Hawajui kitu juu Yake! Yote wajuayo… Je! Wewe ni Mkristo? "Mimi ni Mkatoliki." Je! Wewe ni Mkristo? "Mimi ni Mbaptisti." Je! Wewe ni Mkristo? "Mimi ni Mpresbiteri." Je! Wewe ni Mkristo? "Mimi ni Mpentekoste." Jambo hilo halina uhusiano wo wote na Huo.

Wewe ni Mkristo kwa sababu ya kwamba Mungu, kwa neema Yake, hukuokoa. Nawe unajua jambo Hilo. Na kitu fulani kimeyabadilisha maisha yako, hata unaishi tofauti. Nawe ni mtu mpya na kiumbe kipya katika Kristo Yesu. Hakika.

92 Bali mnaona mahali ulipo ule uzao wa nyoka? Uzao wa nyoka ulikuwa nini? Uzinzi. Mnaelewa? Uzinzi na Hawa. Nini kilichotokea kwa jambo hilo? Ni kitu gani kilichosababisha hilo? Ni kitu gani usiku wa leo?

Angalia nyuma kule ng'ambo, miaka michache iliyopita, wakati ule wimbo wa kwanza ulipotokea. Ninyi wazee, wakati ile… Walikuwa na tabia ya kuzikagua nyimbo kabla hawajaziruhusu kuimbwa redioni. Basi wa kwanza uliotokea, ulikuwa ule wa, "Zikunjeni, enyi wasichana, zikunjeni, mkaonyeshe magoti yenu marembo," na yote namna hiyo. "Wachekeni baba na mama, na muwape wote 'ha-ha-ha!'" Huo ndio wa kwanza waliouruhusu uingie kisiri. Mnafikiri yuko wapi usiku huu yule jamaa aliyeuandika wimbo huo? Yeye amekufa.

Mnafikiri nini juu ya Clara Bow, aliyekuja kwanza na kusema, *"ile mikunjo ya hatari,"* na kule kuvua nguo kulikowapeleka maelfu jehanamu? Mnafikiri yuko wapi usiku wa leo? Amekufa kwa muda mrefu. Yuko wapi, akiwa na huo mwili wake? Umelala kule ng'ambo, umeoza mavumbini, na mabuu na funza yameula yakaumaliza. Nayo nafsi yake imekaa huko ng'ambo mbele za Mungu mwenye haki.

93 Yuko wapi yule mwanamume aliyemchukua mwanamke huyo na kutengeneza nguo hizo za kale zinazoonekana chafu ambazo wao wanazivaa, zinazowabana kwa namna moja ama nyingine, na kuwakaa vibaya? Kwa hiyo wangefanya jambo hilo kwa sababu gani? Unavaa vitu vya namna hiyo kwa sababu gani? Kwa sababu unataka mwanamume akuangalie, na hakuna njia nyingine ya kuthibitisha jambo hilo.

Hivi unajua ya kwamba unapofanya jambo hilo, na maskini mwenye dhambi anakuangalia, unajua ni nini kimetendeka? Kwenye ile Hukumu… Unasema, "Ndugu Branham, mimi ni mwaminifu tu kwa mume wangu niwezavyo kuwa." Utahesabiwa mwenye hatia ya kufanya uzinzi. Yesu alisema, "Kila mtu amtazamaye mwanamke kwa kumtamani amekwisha kuzini naye moyoni mwake." Wakati itakapombidi mtu huyo kujibu kwa kufanya uzinzi, ni nani atakayekuwa amesababisha jambo hilo? Jinsi ulivyovalia na kujionesha.

Naam, sisemi unapaswa kuvaa kama kitu cho chote kile kutoka kwenye sanduku la vitu vya kale. Lakini, unaweza kuonekana zaidi kama mama wa heshima.

94 Nawe unatoka hapa na kutoa nguo, maskini kaptula zako fupi, na kujifunga riboni ndogo namna hiyo; na mtoto wako mchanga mwenye macho kama kisahani cha sigara, huku ukiwa na sigara mdomoni, ukishuka kwenda mtaani. Hufanyi hivyo kwa kusudi jema. Huenda ukawa mwaminifu kwa jambo hilo, lakini ibilisi anakutumia kama chombo kama tu alivyomtumia Hawa.

Kwa nini ni taifa la mwanamke? Kwa maana linaelekea moja kwa moja hata kwenye kutawaliwa na Ukatoliki. Ni kitu gani leo? Kamwe huwasikii wakimtaja Yesu. "Salamu Maria! Mariamu, mama wa Mungu! Mtakatifu Cecilia!" Kila namna ya watakatifu, watakatifu waliokufa. Hapa si muda mrefu uliopita, huko chini katika …

95 Nilikuwa kule Mexico, mwaka jana. Huyu hapa anakuja mwanamke maskini, anajikokota. Magoti yake, yote yanajikokota namna hiyo, na ngozi; analia, huku ameshika mikono yake. Naye baba ameandamana naye, huku amewabeba watoto wawili wadogo, hao wanalia; mama anaugua sana; kwa sababu mwanamke fulani, ambaye wanamwita mtakatifu, alikufa. Walikuwa wameweka sanamu yake juu kule kilimani. Mpenzi fulani alimwua. Na mara tu alipouawa namna hiyo, bila shaka, yeye ni mtakatifu; alikuwa Mkatoliki. Kwa hiyo basi alikuwa anaenda, kufanya vitubio; naye ilimlazimu kujikokota maili mbili, juu ya kokoto, kufanya toba.

Ndugu, kama kuna jambo moja linalonibidi kufanya, Yesu Kristo alikufa bure. Neema, nimeokolewa; na si kwa—kwa nafsi yangu, bali kwa mapenzi ya Mungu, na kwa wema wa Mungu.

96 Hao waandishi wa habari waliniuliza, kasema, "Bw. Branham…" Yu—yule mtoto mchanga aliyekufa alikuwa amefufuliwa, na mambo machache kule. Wakatoliki elfu thelathini … La, samahani. Ilikuwa ishirini elfu. Elfu thelathini ilikuwa Afrika. Wakatoliki elfu ishirini walimpokea Kristo kama Mwokozi wao binafsi, kwa wakati mmoja, wakati jambo hilo lilipotendeka, wakisimama huko kwenye Jiji la Mexico. Basi hao makasisi, wasingeweza kusema jambo lo lote; wengi mno, wangesababisha ghasia. Kulikuwa na wengi sana waliounga mkono. Kwa hiyo akasema, "Bw. Branham, unaamini watakatifu wetu wanaweza kufanya jambo lilo hilo unalofanya wewe?"

Nikijua fundisho lao, nikasema, "Bila shaka, kama wanaishi." Mnaona? Kwa hiyo, huwezi kuwa mtakatifu wa Kikatoliki mpaka uwe umekufa, wajua.

Kwa hiyo akasema, "Loo, huwezi kuwa mtakatifu mpaka utakapokufa."

Nikasema, "Unasoma jambo hilo wapi? Paulo alisema, 'Kwa watakatifu walioko Efeso,' na hao walioitwa na Mungu. 'Kwa watakatifu walioko Efeso,' alikuwa anasoma waraka wake; na hao watakatifu wako mahali pengine, huko Galatia, na—na 'watakatifu walioko Rumi,' na kadhalika. *Watakatifu*, 'waliotakaswa.' Vipi kuhusu hilo?"

97 Yeye alisema, "Bila shaka, sasa, hatupaswi kubishana kwa Biblia. Kwa maana, sisi ni kanisa, na yale kanisa lisemayo. Hatujali Biblia inasema nini. Ni yale kanisa liliyosema." Kasema, "Basi maoni yako ni nini juu ya Kanisa Katoliki?"

Nikasema, "Laiti usingaliniuliza jambo hilo. Kwa kuwa uliniuliza mimi, sasa nitakwambia Kweli."

Kasema, "Vema, ninataka uniambie Ukweli."

Nikasema, "Ibada ya mizimu ya hali ya juu sana niijuayo."

Akasema, "Umepataje jambo hilo?"

Nikasema, "Cho chote kinachowasiliana kwa maombi na wafu ni kiabudu mizimu." Nikasema, "Kama huyo mtakatifu akijibu, basi yeye yuko kuzimu. Kwa maana, hao waliovuka ile njia, Biblia ya—yangu ilisema ya kwamba asingeweza kurudi." Hiyo ni kweli. Nami nikasema, "Kama ndivyo ilivyo, kama yeye alikuwa ni mtakatifu; ni ibilisi akizungumza kama huyo mtakatifu, wala si huyo mtakatifu, hata hivyo."

Naye akasema, "Vema, sasa, kwa dakika moja tu." Kasema, "Unawaombea wafu, pia."

Nikasema, "Wapi?"

Yeye alisema, "Yesu Kristo alikufa."

Nikasema, "Lakini akafufuka tena. Yeye si mfu. Lakini Yeye yu hai, kufanya upatanisho, na mpatanishi pekee kati ya Mungu na wanadamu."

"Mimi ndimi niliyekuwa nimekufa, na ni hai tena, na ni hai milele na milele. Ninazo funguo za mauti na kuzimu." "Yeye atakaye, na aje anywe bure maji ya Uzima." Jamani! Huyo ni Mungu wetu. Huyo ni Mungu wetu.

98 Na uzao wa wenye haki uko karibu kwisha. Nena na watu juu ya mambo haya. Nena na watu kuhusu kurudi kwenye njia ya Biblia. Nena na watu kuhusu miujiza. Nena na watu juu ya jambo hilo. "Kanisa lao haliamini jambo hilo," kwa hiyo wao ni watoto haramu, kwa Mungu. Biblia ilisema kama hatuwezi kuvumilia mateso, na majaribu, dhihaka, na kuitwa "watakatifu wanaojiviringisha" na kadhalika, namna hiyo; kama hamwezi kuvumilia jambo hilo, ninyi ni watoto haramu, na si watoto wa Mungu. Biblia ilisema hivyo.

Niite "mtakatifu anayejiviringisha," ukitaka. Niite chochote unachotaka. Mradi tu moyo wangu uko sawa na Mungu, na ujasiri wangu unalingana na Biblia ya Mungu, ninaendelea moja kwa moja upande uu huu. Naam, bwana. Hivyo ndivyo tunavyoamini. Hilo ni Kanisa la Mungu aliye hai, ambalo haliji kwa theolojia. Haliji kwa mawazo ya kiakili ya kujibunia. Linakuja kwa Kweli yakini iliyofunuliwa ya kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu.

99 Kama nilikuwa tu na wazo la kiakili, kwa maana kanisa la Kibatisti ama kanisa la Kimethodisti lilinifundisha mambo haya kadha na kadha; ninapoisikia Biblia hii, iwapo Biblia… Kama nilikuwa nimebatizwa katika Jina la "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu," na kuisoma Biblia hii, na mhubiri fulani akaniambia ya kwamba hakuna mtu katika Biblia aliyepata kubatizwa ila katika Jina la Yesu Kristo, nami nikaisoma na kuona ya kwamba ilikuwa ni Kweli, ningeingia majini upesi niwezavyo. Naam, bwana.

100 Kama mtu fulani aliniambia ya kwamba—ya kwamba Yesu Kristo alikuwa mponya mkuu; na kanisa langu liliniambia, "Siku za miujiza zimepita," nami nilikuwa na haja ya kuponywa; ningekimbia upesi nilivyoweza, madhabahuni, nipate kuponywa. Hakika ningefanya hivyo.

Kama nilikuwa mhubiri, na nilikuwa na mhubiri mwa— mwanamke mimbarani mwangu, ndipo nisome katika Biblia ile na kuona ya kwamba mwanamke hakupaswa kuhubiri, ningemwondoa hapo, hata kama jambo hilo linichune ngozi.

Basi kumbukeni, akiketi moja kwa moja kule nyuma aliko Dada Wright, usiku mmoja, ya kwamba mwanamke fulani alikuwa anataka kunitupa nje ya mlango kwa kufanya jambo kama hilo. Naam, bwana. Nikasema, "Hutaingia kanisani mwangu ukiwa na ninii yako ya kale…" Wakati walipokuwa wanavaa, ama kukata nguo zao huko chini kabisa namna hii, na kitu hicho cha kuchekesha, na karibu nusu ya mwili wao ni uchi. Nikasema, "Wakati wo wote wakija kanisani mwangu, hakika nitawatoa nje." Na maskini kipusa wa kale chini huku, alikufa si muda mrefu baada ya hapo; naye akaniita, akifa. Alikuwa msichana wa Kikatoliki, akaenda pale akaketi chini na kitu hicho namna hiyo. Niliangalia nyuma nikamchunguza, ameketi hapa juu, nao walikuwa wanaimba. Nikavua koti langu, nikaenda kule nyuma, nikaliweka mabegani

mwake. Nikasema, “Mama, kama utanisikiliza nikihubiri, tafadhali vaa koti hili ukiwa katika kanisa la Mungu.” Mnaona? Hakika.

101 Akatoka hapo kwa vishindo, na kubenua maskini midomo hiyo juu. Akatoka nje ya jengo. Akatoka jengoni. Akasema, “Iwapo ana dini, nisingemruhusu ng'ombe wangu apate dini ya namna hiyo.”

Nikasema, “Usijali, hataipata.”

Kisha tulikuwa na lile hema, wakaniita alipokuwa anakufa. Alikuwa na ugonjwa wa mshtuko wa moyo, naye alikuwa anakufa. Mumewe akaja. Akasema, “Njoo upesi!” Nami nilikuwa katikati ya mkutano. Mvulana mkubwa, mrefu, akisimama mlangoni, akiningojea. Nami nikakimbia kama …

Nikaingia kwenye gari langu na kukimbia huko nje. Nilipokuwa nikipanda, nikakutana na nesi yule mzee kule, ambaye anaishi Howard Park, hata sasa. Akasema, “Kasisi, hakuna haja ya kuja.” Hilo limekuwa yapata miaka ishirini iliyopita, labda mingi kidogo. Kasema, “Amekufa.” Kasema, “Amekufa yapata dakika tatu.” Kasema, “Alipiga makelele kwa nguvu alivyoweza, akikuita.” Kasema, “Nina ujumbe wako.”

Kasema, “Wa nini?”

Kasema, “Mwambie mhubiri yule, niliyenena habari zake, 'Tafadhali nisamehe.'”

102 Nikashuka huko kumwangalia. Mwanamke mwenye sura nzuri; naye alikuwa ameugua sana. Alikuwa na madoa madogo puani mwake; mwanamke anayependeza. Nayo hayo madoa, yalionekana kama kwamba, yalitokeza. Na macho yake yalikuwa yametokeza nje kabisa kwenye matundu yake, nayo yalikuwa yamerudi nyuma nusu. Bila shaka, matumbo yake na figo zilikuwa zimesogea, na mvuke unatoka kila mahali kitandani, namna hiyo.

Ndipo mumuwe akaniangalia, kasema, “Ndugu Branham, sema sala, maana alitaka kukuona wewe.”

Nikasema, “Maombi kwa ajili yake sasa hayatamfaa kitu.”

“Mti unavyoegemea, hivyo ndivyo jinsi unavyoanguka.” Mnaona? “Msidanganyike; Mungu hadhihakiwi. Cho chote apandacho mtu, ndicho atakachovuna.”

103 Mnaona mahali lilipo? Sasa jambo gani limetukia? Angalia mwanamke ambaye angefanya jambo hilo. Waangalie wanawake walioishi kule nyuma, mwiimba dansi, bintiye alikuwa ni nani? Mlimbwende. Binti wa mlimbwende ni nani? Tineja mcheza rumba. Binti yake atakuwa nini? A-ha! Ni kitu gani?

Mnaona uzao wa mwenye haki?

Jiangalieni enyi Wabatisti. Rudini nyuma muda kidogo uliopita. Rudini nyuma kwa John Smith, mwanzilishi wenu, enyi Wabatisti. Wakati, yeye alipoomba kwa ajili ya uovu wa watu, mpaka, yeye aliwalilia na kuwaombea watu mpaka macho yake yakafunga kwa kuvimba, na ilimbidi mke wake kumlisha mezani, kiamshakinywa chake.

104 Pia ninyi Wamethodisti mlio hapa karibu, huku mmevalia lulu puani mwenu na maskioni mwenu, na mnaonekana kama tandiko la ibilisi la kukalia; na mnatoka nje, mmevaa kaptula, na takataka kama hizo! Wakati, mzee John Smith, mmoja wa wazee wa kanisa la Kimethodisti, kabla hajafa mwenye umri wa miaka themanini na mitano, alihubiri somo fupi la miaka minne…masaa manne. Iliwabidi kumchukua na kumweka mimbarani. Na haya hapa maneno yake ya mwisho. Alisema, “Nimeshtushwa sana na tendo la kanisa la Kimethodisti.” Kasema, “Hata binti za kanisa la Kimethodisti wanavaa pete za dhahabu vidoleni mwao.” Angesema nini sasa, wakivaa kaptula, na kuimba kwenye kwaya?

Mlikimbia vizuri. Nini kilitukia? Mnatenda kama mama yenu. Hiyo ni kweli kabisa.

Hiyo ndiyo sababu hatutaki yo yote ya madhehebu haya yakining'inia karibu na haya, ama kushikizwa hapa, “Sisi ni Wamethodisti. Sisi ni Wabaptisti.” Sisi ni wa Kristo tu. Liacheni namna hiyo, na iweni huru.

105 Sasa, mnaona uzao wa nyoka? Mwanamke kama huyo angelipa nini hivi sasa? Jambo hilo lingefanya nini? Nini? Waliendelea tu, wakija moja kwa moja. Waliwasukuma Wabatisti nyuma, wakawasukuma Wamethodisti nyuma, wakawasukuma Wapresbiteri nyuma. Wangefanya nini? Wote walirudi moja kwa moja, kama mama yao, yule kahaba wa kale. Hao hapo wote, wakifanya ukahaba ule ule. “Vema, haileti tofauti yoyote. Wamekwisha zamishwa majini. Wamekwisha nyunyiziwa maji. Wao, wao wamekuja, wakaungama. Wamechukua miezi yao sita ya kufunga; hawakunywa sana mnamo wakati huo, na kadhalika. Walikuwa wafuasi wazuri. Wao wanalipa vizuri kwenye…” Loo, jamani! Hilo halina uhusiano wo wote na matunda ya Roho.

Matunda ya Roho ni “imani,” kumwamini Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele; “Upendo” kwa ndugu; “Furaha, amani, uvumilivu, wema, utu wema, saburi, upole, kiasi.” Hayo ndiyo yale mambo, matunda ya Roho.

106 Nasi tunamchukua mtu, "Vema, yeye—yeye anaishi maisha mazuri katika ujirani." Vivyo hivyo na Esau.

Esau hakumdhuru mtu ye yote, na Esau alikuwa wa ibilisi; bali Yakobo, kutoka katika tumbo lile lile la uzazi, alikuwa ni wa Mungu. Uzao wa ibilisi; Uzao wa mwanamke, ndiko Uzao wa Mungu ulikopitia.

Sasa, mnaona, yote yamefikia kwenye jambo hili, limebakia nini ulimwenguni leo? Nitasema jambo hili kwa ukali hasa, kulisisitiza hili, ndipo tutaanza ufufuo baada ya jambo hili, katika mkutano ufuatao. Imefikia kwenye umbo fulani. Na, tafadhali, sisemi jambo hili kwa kukufuru. Silisemi kusudi niwe mkorofi. Imefikia mahali fulani, kwenye kundi kubwa la watoto haramu na wa dini. Hayo hapo matamshi yangu ya mwisho. Hapo ndipo imefikia kabisa sasa. Mnajua kwamba jambo hilo ni kweli. Imefikia mahali mpaka ni kujiunga na kanisa na kuwa wafuasi wa kanisa, "Wenye mfano wa utauwa, wakikana Nguvu zake," hata imefikia kwenye kundi la watoto haramu wa dini. Hivyo ndivyo ilivyo hasa.

107 Ni nini kingine kinachosalia? Kuna kombora linaloning'inia kule ng'ambo, mengi, mabomu hatari na kila kitu. Yanangojea tu zile nguvu zifike. Ndipo kutakuweko na maangamizi ya moto, kama kulivyokuwa na ya maji.

108 Basi, marafiki, lo lote mfanyalo, kama wewe ni Mkristo na una Mungu moyoni mwako, nawe unajua ya kwamba umepita kutoka mautini kuingia Uzimani, unapaswa kuwa mtu aliye na furaha sana duniani kote. Wakati Roho Mtakatifu ndani yako …

Wakati, Biblia inasema, "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele."

Madhehebu yanasema, "Lakini tunaamini miujiza imepita."

Roho Mtakatifu anasema, "Amina. Yesu Kristo ni yeye yule jana, na hata milele. Na iwe hivyo."

109 Kama Biblia ilisema, "Tubuni, mkabatizwe kila mmoja wenu katika Jina Lake Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi zenu, mtampokea Roho Mtakatifu. Kwa maana ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, kwa Mataifa, wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie." Mnaona? (Si, "wote watakaoitwa na Wamethodisti, watakaoitwa na Wabatisti.") Lakini, "Wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie, watampokea huyu Roho Mtakatifu, na kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo." Ni vile Biblia ilivyosema.

Wakati hilo linapokugusa, unasema, "Amina."

Kanisa lilisema, "Loo, haileti tofauti yoyote."

Lakini huyu Roho Mtakatifu ndani yako, aseme, "amina" kwa Neno Lake. "Mtu hataishi kwa mkate tu, bali Neno litokalo katika kinywa cha Mungu." Haya basi.

110 Nataka mnioneshe Andiko moja ambapo lilisema tofaa lilianzisha jambo hili sasa. Ninawatakeni mnioneshe kwamba wanakula matofaa. Nimewaonesha ambapo Kaini alifikiria jambo lile lile, na ambapo uzao wake ungali unawazia jambo lile lile.

Lakini ufunuo wa kiroho wa Mungu unathibitisha, kwa Biblia, ya kwamba ilikuwa ni kujuana kimwili kati ya mwanamume na mwanamke, bila ruhusa. Hapo ndipo wanefili wenu walipotokea. Hapo ndipo dhambi yako ilipotoka. Hapo ndipo ufisadi wako ulipotoka. Hapo ndipo iliposhukia.

Sasa angalia katika yote haya—haya, angalia, nyo—nyoka alikuwa mwerevu mara mbili. Uzao wake daima umekuwa mwerevu mara dufu. Nami ningetaka kupanda kwenye mimbara hii na kushika maikrofoni hii mkononi mwangu, [Ndugu Branhama anasogeza maikrofoni—Mh.], na kubandika miguu yangu juu ya mimbara, na kusema jambo hili. Pia, siku hizi, wako wapi majitu yenu wenye bongo? Mchungaji wenu ambaye ameshuka akaenda akapata maarifa mengi sana ya kiakili, naye anasimama; yeye ni mchungaji wa makanisa yaliyo makuu sana nchini, na kadhalika namna hiyo. Uzao wa nyoka unasimama wapi? Katika sehemu zenye akili nyingi kama hizo; wasomi werevu, wajanja. Hapo ndipo alipo. Hapo ndipo alipo.

"Si kwa nguvu, wala kwa uweza, bali kwa Roho Wangu, asema Bwana." Mnaona? Hapo ndipo wewe …

111 Kisha unamchukua maskini ndugu mdogo anayesimama pale pembeni, akilia sana, na labda akisimama kule chini akipiga gita ya kale, akisema, "Ndugu, njoo, ukamtafute Bwana!"

Mchungaji anatembea pale, aseme, "A-ha! Nisingeruhusu kusanyiko langu… Mbona, nisingejihusisha, nisingeruhusu ninii wangu…nisingetaka Liddy na Johnny na hao wengine wanione karibu na mahali kama hapo." Endelea, ewe uzao wa ibilisi, unaelekea kwenye kikomo chako cha Milele, kwa vyo vyote. Hiyo ni kweli. Ningeweza kusema neno lingine pale, na kusema, "watoto haramu," na hapo ndipo ambapo imekaribia kufika. Kwa kuwa, mnaona, ninyi…

"Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu. Na wote wanijiao Mimi, nitawafufua katika siku ya mwisho. Hakuna kitakachopotea. Ninacho. Nitakiweka. Hakuna mtu anayeweza kufanya

jambo hilo, isipokuwa Huyu."

Yote yako Kwake. Huwezi kusema, "Nimefanya jambo moja." Ni neema ya Mungu ambayo imelifanya jambo hilo lote. Kwa hiyo, hakuna kitu nilichofanya. Kamwe sikuwa na jambo la kufanya; wewe kamwe, wala. Hukustahili hata jambo moja. Mungu alifanya kila sehemu yake. Kamwe hujageuza kidole chako kwa sehemu moja yake. Wewe hukusema, "Vema, nilitoka kwenye jamaa nzuri. Nilifanya jambo *hili*." Hilo halina uhusiano wo wote na jambo hilo. Mungu Ndiye aliyefanya jambo hilo; Rehema ya Mungu.

112 Ninasikitika sasa, saa tano haijafika kabisa bado, bali nitamaliza, kwa vyo vyote. Mnaona?

Ni wangapi wanafahamu ya kwamba Biblia inanena juu ya mambo haya kwamba ni Kweli; ninyi watu wa Maskani ya Branham, hasa? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Sasa, hiyo ni kama moja tu ya kumi na sita ya yale tunayofundisha na kuamini. Lakini, kumbukeni, kwenu mliohudhuria, huenda nikasema jambo hili, enyi watu msiokuja hapa kama washiriki. Jinsi tunavyoamini jambo hili, ya kwamba Hii ni Biblia, na Biblia ni Kweli ya Mungu.

Nasi tunaamini, ya kwamba, katika Agano la Kale, sasa, walikuwa na njia ya kujua lililokuwa kweli na lisilokuwa kweli.

Sasa, sote tunajua ya kwamba walikuwa na torati iliyoandikwa. Ni wangapi wanaojua jambo hilo? Torati, zile— zile amri zilikuwa kwenye lile sanduku, na kadhalika; sawa, na torati juu ya zile amri. Kasema, "Usizini. Kila mtu anayezini anapigwa mawe." Mnaona? Hiyo ilikuwa ni ile—ile amri, na torati juu ya amri. Sasa, lile sanduku lilikuwa limekaa namna hii; zile amri zilikuwa mle ndani, na zile torati za zile amri zilikuwa kwenye mifuko iliyokuwa upande mmoja wa lile sanduku. Kama mtu alishuka hapa, akafanya uzinzi; waliangalia chini hapa kuona vile sheria ilivyosema, "mpigeni mawe." Walimtoa nje moja kwa moja na kumpiga mawe. Hivyo ndivyo sheria ilivyokuwa juu ya ile amri.

113 Sasa walikuwa na njia mbili zaidi za kujua. Daima kuna tatu, kama thibitisho. Walikuwa na njia nyingine ya kujua, na hiyo ilikuwa ama kwa nabii ama kwa mwotaji. Ni wangapi wanaojua jambo hilo? "Kama kuna mmoja miongoni mwenu aliye wa kiroho, ama nabii, Mimi Bwana nitajitambulisha kwake katika ndoto, na kunena naye katika maono." Hiyo ni kweli. Sasa, yeye alikuwa mtabiri.

Sasa, kama mtu anakuja hapa, kasema, "Loo, Haleluya, nimelipata! Ninatabiri sasa katika Jina la Bwana. Nina ufunuo." Hawakuruhusu jambo hilo liende namna hiyo, kama ninyi watu mnavyofanya. Walichunguza hilo kwa Mungu, kwanza.

114 Sasa, kwenye kifuko cha kifuani cha Haruni walikuwa na kile walichokiita Urimu Thumimu. Ni wangapi waliopata kusikia neno hilo? Ilikuwa ni kitu gani? Yalikuwa mawe kumi na mawili, sita kwa kila upande, ya wale wazee wetu kumi na wawili; yaspi, Yuda, na kadhalika, na kuendelea moja kwa moja, yale mawe kumi na mawili. Kisha wakamchukua nabii huyu, ama mwotaji, ndipo wakakitundika pale juu kifuko hiki cha kifuani, nao wakamsimamisha pale. Basi wakasema, "Sasa tabiri na ueleze unabii wako."

"Bwana alinena nami na kusema mambo fulani—fulani."

Haidhuru ulionekana dhahiri namna gani, huenda ukasikika kana kwamba ni kweli kabisa; bali kama nuru hizo hazikuungana na kufanya rangi ya upinde wa mvua ukakingama pale, ile Urimu na Thumimu, nuru hizo zikichangamana pamoja, ya kimbinguni yakitenda kazi, kuthibitisha. Mnaona, Mungu daima amethibitisha Neno Lake. Mnaona? Basi iwapo nuru hizo za kimbinguni hazikumulika pale, basi sijali ulionekana halisi jinsi gani, ulikuwa ni kosa.

115 Kama mwotaji alisema, "Niliota ndoto, na ndoto hii ilisema, ya kwamba, 'Israeli wanapaswa kuondoka waende mahali fulani, maana Waashuri watakuja upande huu na kuuzingira.'" Walimchukua yule mwotaji kule chini; alisimulia ndoto yake. Kama nuru hizo hazikumulika kule, alikuwa amekosea, haidhuru vipi… Kama Waashuri walikuwa tayari wameketi kule vitani, alikuwa amekosea. La, bwana. Wao, kabisa, ilibidi kuthibitishwa na Urimu Thumimu.

Sasa kila mtu anajua ule ukuhani wa kale ulikuwa umeondoka, umeondolewa, na Urimu na Thumimu ikaondoka pamoja nao. Tunajua jambo hilo, sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.]

Na ukuhani mpya ukaingia. Nini? Je! Tuna Urimu Thumimu leo? Naam, bwana. Neno la Mungu! Naam, bwana. *Ndilo* hili. Kama mtu ye yote ana ufunuo wa namna yo yote, ama anazungumza jambo lo lote, ama fundisho lo lote ambalo haliambatani na ku-…na kukubaliana na Biblia hii, kote kote katika Maandiko yote, amekosea. Sijali ni wa madhehebu gani, ni mzuri vipi, ni mwerevu vipi, ameelimika vipi; amekosea.

116 Na wakati mtu ye yote anakwambia mambo haya, ambayo tumefundisha hapa kanisani sasa, na anakwambia, ya kwamba, "Kama umenyunyiziwa, ni sawa," yeye amekwambia uongo. Hilo halitamulika kwenye Urimu na Thumimu. Wakati anapokwambia, ya kwamba, "Kumwagiliwa ni sawa," amekwambia uongo. Akikwambia, "Kubatizwa katika jina la 'Baba, Mwana, Roho Mtakatifu,' ni sawa," amekwambia uongo. Kama akikwambia, "Siku za miujiza zimepita," amekwambia uongo. Kama akikwambia, "Ni sawa

kwa wanawake kuhubiri," amekwambia uongo. Kama akikwambia, "Ni sawa kwako kuendelea na kushikamana na madhehebu yako," amekwambia uongo. Halitamulika kwenye Urimu na Thumimu. Na mambo dazani yanayotoka, ndani ya huyo "MAMA KAHABA" wa kale, na kushuka kule, na hiyo ndiyo sababu tunakaa mbali na madhehebu.

117 Tunawapenda ndugu zetu na dada zetu huko nje kwenye madhehebu hayo. Bali huendi, na kusema, "Mimi ni Mmethodisti," na kukufanya Mkristo, kwangu mimi. Wewe ni Mkristo kwa sababu umezaliwa na Roho wa Mungu. Si lazima uwe Mmethodisti ama Mbatisti. Si lazima uwe wa hili wala lile. Inakubidi kuzaliwa tu na Roho wa Mungu. Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.]

Kwa misingi hii, kama mtu ye yote yuko hapa na anataka kushirikiana na kuingia katika ushirika wa ibada hii, naye anataka kuwa—anataka kuzamishwa, kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo, hiki hapa kisima. Watabatiza, katika dakika moja tu.

Kama kuna mtu ye yote, wengi hapa, mtu ye yote anayetaka kuja, katika njia nyingine yo yote? Tuko hapa. Hiyo ni kweli.

118 Sasa, sisi—sisi hatuna uanachama wowote; unakuja tu hapa kwenye kanisa hili. Tunaamini ya kwamba Kristo yuko katika kanisa la Kimethodisti, kanisa la Kibatisti, kanisa la Kipresbiteri. Yeye ana washiriki katika kila moja la hayo. Na kitu kinachokosekana, leo; ni unabii wa uongo ukitoa mambo hayo nje, mafundisho ya makanisa hayo, ambayo yanapingana kabisa na Biblia.

Naam, kama mtu ye yote angelifanya jambo Hilo dhahiri hivyo kwangu, hakika ningejifanyia mimi mwenyewe… Ninaamini kuna Roho wa Mungu wa kutosha ndani yangu, kuichunguza Biblia hiyo na kuja na kulisahihisha jambo hilo. Kama niliondoka tu nikaenda nikampa mhubiri mkono, na kuandika jina langu kwenye kitabu, na bado nimekuwa na chuki na kijicho moyoni mwangu, na ningali nilikuwa na wivu na ugomvi, na ningali simwamini Yesu Kristo kuwa mponya mkuu, na kadhalika namna hiyo, ningeondoka niende kunyosha mambo na Mungu, upesi sana. Hakika ninaamini ningefanya hivyo. Ni—ningekuwa mwaminifu kuhusu jambo hilo. Ningeenda kujipatanisha na Mungu. Kama nilijishikiza tu kwa sababu nilikuwa Mbatisti ama Mmethodisti, ningeshuka niende nikapate Ukristo moyoni mwangu. Ningefanya hivyo. Naam, bwana.

119 Sasa kumbukeni uhamsho unaokuja, ambao utaanza, Bwana akipenda, Jumatano hii ijayo usiku. Ni juu ya msingi huu.

Sikilizeni, enyi marafiki, kuna Mungu wa kweli na aliye hai. Hiyo ni kweli. Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu. Roho Mtakatifu yumo Kanisani leo.

Sasa, kama niliambiwa tu na mtu jambo hilo, ningekuwa na haki ya kulitilia shaka. Lakini, sikilizeni. Siku moja huko ng'ambo, kama mvulana mdogo, nilikuwa mimesimama chini ya mti; nami nikamwona Yeye. Nilimsikia. Akaniambia, akasema, "Jiepushe na hao wanawake wabaya. Jiepushe na sigara. Jiepushe na kulaani, kunywa pombe, na mambo haya yote. Nina kazi utakayofanya utakapokuwa mtu mzima." Ninajua Yeye ni Mungu halisi, anayechukuana na Neno Lake.

120 Nilipokuwa mkubwa kidogo, jinsi alivyokutana nami, jinsi alivyosema nami! Jinsi nimemwona huko ng'ambo, kama kijiti kinachowaka moto, na Moto huo ukisogea kule ng'ambo! Jinsi nimemwona akinena na kusema yale hasa yangetukia; na, kila wakati, yanatukia kikamilifu yawezavyo kuwa, kikamilifu namna hiyo.

Yeye yule yule anayesema mambo hayo makamilifu namna hiyo, ni Yeye Yule Ambaye hunivuvia kufundisha Biblia hii jinsi tu ninavyoifundisha. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo, linatoka kwa Mungu. Kwangu mimi, ni Mungu Mwenyezi, Naye ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

Yesu alisema, "Ninatoka kwa Baba, na ninaenda kwa Baba." Wakati alipokuja …

Wakati Yeye alipokuwa Mungu nyikani, Yeye alikuwa Nuru imulikayo. Na ni wangapi wanaojua jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Yeye alikuwa Nuru inayowaka, Nguzo ya Moto.

Naye akaja hapa duniani, Naye akasema, "Nilitoka kwa Baba, nami ninaenda … Nimetoka kwa Mungu, nami ninarudi kwa Mungu."

121 Wakati alipokufa, akazikwa, akafufuka tena, na Paulo akienda zake Dameski akakutana Naye tena, Yeye alikuwa ni nani? [Mtu fulani anasema, "Nguzo ya Moto." — Mh.] Bado ni Nguzo ya Moto. Naam, bwana.

Yeye alifanya nini alipokuwa hapa duniani? Alifanya nini alipokutana na Paulo? Yeye alimtumaje? Yeye alimtuma kwa nabii aliyemwambia jinsi ya kubatizwa, akamwambia la kufanya; akaweka mikono yake juu yake na kumponya, akamwambia alikuwa ameona ono.

Yesu yule yule yuko hapa leo, akifanya mambo yale yale, na bado ni Nguzo ile ile ya Moto,

akifundisha jambo lile lile, na kulithibitisha kwa Neno Lake, na kwa ishara na maajabu. Nina furaha sana kuwa Mkristo, sijui la kufanya. Nina furaha kwamba wewe ni Mkristo.

122 Na ninyi, maskani hapa, niliwaambia tutabadilisha jina la hili. Si sahihi kwake kuwa Maskani ya Branham. Huyo ni mtu tu, mnaona. Tutabadilisha jina lake, tufanye jina lingine. Tutalifikia hilo, baada ya kitambo kidogo. Ninataka tu li—liwe kanisa la Mungu aliye hai. Sitaki Wamethodisti, Wabatisti, Wapresbiteri, Wapentekoste. Mimi …

123 Watu hao wote, ninawapenda kwa moyo wangu wote. Sijui nani ni nani. Siwezi kuwaambia. Sina budi kuhubiri tu Neno. Ninatupa jarife na kulivuta. Kuna vyura, na kuna buibui wa maji, na kuna nyoka, na kuna samaki, pia. Hiyo ni juu ya Mungu kuamua jambo hilo. Ninavuta tu wavu, ninahubiri tu Neno na kuliingiza ndani, na kusema, "Hawa hapa, Bwana, kote madhabahuni. Unawajua walio Wako; Umewajua tangu kuwekwa misingi. Sijui nani ni nani. Unafanya hivyo, kwa hiyo ni juu Yako, Bwana. Hilo ndilo bora niwezalo kufanya. Nitaenda hapa na kuvua mahali pengine sasa, na kuingiza kundi lingine. Hayo tu ndiyo ninayoweza kufanya." Vema.

Loo, najisikia kuendelea na safari,
Najisikia kuendelea na safari;
Makao yangu ya Mbinguni yanang'aa na mazuri,
Na najisikia kuendelea na safari.

124 Sasa kumbukeni, mtu ye yote anayetaka kuonana nami, mpigie tu simu Bw. Mercier hapa, ama BUtler 2-1519. [Namba ya simu imebadilishwa. — Mh.] Tutafurahiwa kukuona. Kama wapenzi wako wakija, ikubidi kuondoka haraka mnamo wakati wa ufufuo… Sasa ninaondoka, tangu usiku wa leo, kwenda nikawe peke yangu, na niondoke kwa siku mbili sasa, niwe peke yangu.

Ninaingia tu mle ninaanza kusoma, namna hii, "Bwana, uko karibu nami. Ninajua Wewe uko hapa. Na Neno Lako lilisema utawakaribia hao wakukaribiao." Ninaendelea kuomba na kuangalia mpaka nione ile Nguzo ya Moto ikianza kusogea. Ninajua iko tayari basi. Ndipo ninaenda jukwaani kwa ajili ya ibada ya uponyaji, kuomba, na kufanya kile niwezacho kuwasaidia wagonjwa na wanaoteseka.

125 Tunashukuru kwa wema wako wote sasa. Nanyi mjapo, njoni mkiamini, nasi tunakusudia kuwa na mkutano mkuu. Ninataka kusema ya kwamba …

Ndugu Jeffries, yupo hapa usiku wa leo? Tunataka kumfurahia Ndugu Jeffries na kazi yake. Nadhani amerudi visiwani, na kadhalika.

Ninafurahi kuwaona Ndugu na Dada Wright, na wengi wenu ninyi watu hapa.

Nami nilimwona wakili Robertson hapa, muda mfupi uliopita, akiingia muda kidogo uliopita. Nilitaka kumpongeza kwa—kwa ujumbe wake aliokuwa nao juzijuzi. Hakuna mtu aliyesema ni nani. Hiyo ilikuwa ni aibu. Alikuwa na ujumbe mzuri sana juu ya unabii, kitu kama nilichokuwa nikihubiri usiku huu.

Basi, kwa hiyo, halafu kulikuwa na mhudumu mwingine hapa asubuhi ya leo, ama usiku wa jana, Ndugu Smith, kutoka kanisa la Kimethodisti…ama kutoka kanisa la Mungu, huku. Sijui kama yuko hapa usiku wa leo, ama hayuko. Kama ukiwahi kusimama kwenye mimbara hii na kuangalia nyuma upande ule, kwa namna fulani ni vigumu kujua; ni tambarare, unaona, na huwezi kujua. Kama uko hapa, Ndugu Smith, tunakufurahia.

126 Basi huyu, anayeketi papa hapa, maskini ndugu huyu kutoka Georgia, papa hapa nyuma ameketi karibu na Ndugu Collins? [Ndugu Neville anasema, "Naam." — Mh.] Nina furaha kukuona hapa tena usiku wa leo, ndugu.

Na ninyi wengine, ninyi nyote, kila mmoja anajua wewe ni nani.

Ninaamini huyu ni yule dada na ndugu hapa ambao walienda na kumwombea yule msichana wakati ule, papa hapa, daktari anayeketi hapa kando. Bwana akubariki, daktari.

127 Sasa, tafadhali msijisikie kukasirishwa nami, ninyi wahudumu na ndugu, kwa sababu jinsi ninavyolikemea hili kwa bidii niwezavyo. Hii ndiyo maskani yetu. Hayo ndiyo tunayotetea, nasi tunataka kuiweka moja kwa moja kwenye Neno hilo, na kuwatikisa Kwalo. Halafu, kama ukipata kutoka mstarini, tutarudi na kusema, "Ulijua vema zaidi. Hii hapa kwenye kanda." Mnaona? Haya basi. "Hili hapa kwenye kanda."

Tuna mengi sana zaidi tunapaswa kuyaendea, kule, Leo. Lakini, lakini sisi … Una kiasi hicho. Dumuni moja kwa moja na Hayo, nasi tutapata yaliyosalia baada ya kitambo kidogo. Kama vile yule mtu alivyokuwa, akila tikiti maji, kasema, "Hilo lilikuwa tamu sana, bali kuna jingine zaidi la hilo." Kwa hiyo tuna mengi zaidi Yake, bado, yanayokuja.

128 Bwana awabariki, vizuri sana sasa. Wakati sisi … Nitafanya ibada ya ubatizo sasa hivi. Hiyo ni kweli, Ndugu Neville? [Ndugu Neville anasema, "Naam, ninaamini hivyo." — Mh.] Kuna mtu hapa wa kubatizwa

sasa hivi? Hatujali wewe ni nani; tuko—tuko hapa kubatiza. Inueni mikono yenu, wale waliopaswa kubatizwa. Mtu fulani, naamini ilikuwa … Huyu hapa bibi hapa. Na kulikuwa na mtu mwingine yeyote? Sasa, tuna nguo hapa kwa ajili ya wanaume na wanawake.

129 Sasa, hatusemi, "Ondokeni kwenye kanisa la Kibatisti. Acha kanisa la Kimethodisti." Hatusemi. Rudi moja kwa moja kanisani mwako. Lakini kama hujabatizwa kulingana na Maandiko, katika Jina la Bwana Yesu … Si katika Jina la "Yesu" tu, sasa. Katika Jina la "Bwana Yesu Kristo," hayo ni Maandiko. Umebatizwa vibaya.

Sitaki shida yo yote nitakapofika mtoni. Ninataka kila kitu kiwe dhahiri nijuavyo, ninaposhikilia hiyo tiketi, mnaona, maana ninataka kupanda meli wakati ule. Ningewashauri mfanye vivyo hivyo.

Rudi kanisani mwako. Hilo ni juu, kati yako na Mungu. Hivyo ndivyo tu ninavyoweza kuwaambia.

Lakini hakuna mtu katika Maandiko aliyewahi kubatizwa kwa njia nyingine yo yote ila Jina la "Bwana Yesu Kristo." Na hao waliobatizwa, waliamriwa na Mtakatifu Paulo, aliyesema, "Kama Malaika alihubiri jambo lingine lo lote, na alaaniwe." Akawaamuru waje wakabatizwe tena, mara nyingine, katika Jina la "Bwana Yesu Kristo." Hiyo ni kweli. Naye akafanya jambo hilo. Basi alilofanya, alituagiza kufanya; na jambo hilo ndilo tutakalofanya, Mungu akipenda.

Tunaamini katika kutawadhana miguu. Tunaamini katika ushirika.

130 Tunaamini katika Kuja kwa pili kwa Kristo, mwili unaoonekana wa kibinadamu wa Bwana; si Roho, bali mwili wa kibinadamu wa Bwana Yesu akija tena katika utukufu.

Tunaamini katika kufufuka kimwili kwa wafu, kupokea mwili, si mzee na wenye makunyanzi kama tunavyoenda kaburini; bali mpya, katika kipeo cha furaha ya ujana, tukaishi milele.

Tunaamini katika kutokufa kwa nafsi, kabisa. Tunaamini kuna aina moja tu ya Uzima wa Milele, na huo ndio Uzima unaopata kutoka kwa Kristo Yesu. Hiyo ni kweli kabisa.

Kwa hiyo, hatuamini adhabu ya Milele. Tunaamini katika moto wa jehanum, kiberiti kinachowaka moto, bali hatuamini unaungua milele; kama ukifanya hivyo, una Uzima wa Milele. Kuna Uzima mmoja tu wa Milele; Huo huja kutoka kwa Mungu. Na hiyo ni kweli. Utachomwa moto, labda kwa miaka milioni moja, miaka milioni kumi, sijui, bali huwezi kuwa na Uzima wa Milele. Huwezi kuwaka milele … Unaweza kuungua milele, bali si Milele dawamu. Mnaona, kuna tofauti kati ya Milele dawamu na milele. Milele ni milele na milele, kiunganisho, inamaanisha "muda wa wakati." Lakini, Milele dawamu, huna adhabu ya Milele dawamu.

Una Uzima wa Milele, maana kuna aina moja tu ya Uzima wa Milele. Na yeye aliye na Uzima wa Milele, anaishi na amebarikiwa na Mungu milele.

"Bali nafsi itendayo dhambi, mtu huyo ataninii …" Nini? [Kusanyiko linasema, " … kufa." — Mh.] Hiyo ni kweli. Halafu, haina Uzima wa Milele. Hakika. Ina—ina adhabu yake, bali si Uzima wa Milele.

Kwa hiyo, mnaona, kuna mambo mengi bado ya kufundishwa, tutayapata baadaye. Bwana awabariki.

131 Sasa hebu na tuimbe wimbo huu mzuri wa kale, wakati dada yetu anaenda kule. Ninaamini mama huyu hapa anaweza …

Rosella, huyo ni mama yako? [Dada Rosella anasema, "Naam." — Mh.] Mbona, barikiwa moyo wako! Ninafurahi kukuona, dada, ukifanya jambo hilo. Hilo ni zuri sana.

Rosella Griffin, mmoja wa marafiki wazuri sana tuliopata kuwa nao. Yeye ni kijana mwanamke aliyekuwa na ugonjwa wa ulevi; kwa baadhi yenu enyi watu hapa, huenda akawa ni mgeni. Rosella hajali nikisema jambo hilo. Alipokuja jukwaani kule kwenye—kwenye mahali ambapo…huku Indiana. Kama umewahi kuona sikrepa ya mtu, alikuwa mmoja wao, mlevi wa kupindukia. Ambapo, madaktari wanne wakuu wa Chicago walisema yeye ni … Shirika la Walevi, na wengine wote, walimkatia tamaa. Bali usiku mmoja alipokuja mkutanoni, Roho Mtakatifu aliyaeleza maisha yake na kumwambia papo hapo. Hilo lilitosha.

Mwangalie sasa, nafikiri, mwenye umri wa miaka thelathini na kitu, angefikiriwa ni wa kumi na minane; kijana mwanamke mzuri na wa kupendeza. Hajaonja wiski tangu wakati huo; hana tena tamaa yake. Anamwishia Kristo, akipita mitaani, kila mahali, akishuhudia utukufu wa Mungu, kwa wenye dhambi na walevi wa kupindukia, kote kote katika vichochoro, ko kote kule, kila mahali Chicago, akifanya jambo fulani kwa ajili ya Bwana.

Alibatizwa katika Jina la Bwana Yesu, na mamaye anakuja usiku wa leo kufanya jambo lile lile; kama Mungu aliweza kumponya, kama Yesu aliweza kumponya… "Lo lote mfanyalo kwa neno ama tendo, fanyeni yote katika Jina la…" [Kusanyiko, "…Yesu Kristo."] Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema. Hiyo ni kweli.

132 Vema, sasa tutakuwa na ibada ya ubatizo. Tutazima taa kwa dakika chache tu tunapojitayarisha kwa ajili ya ibada, kubatizwa, ha—halafu basi tutatarajia wakati mzuri katika Bwana.

Je! Mtafanya ibada ya ubatizo usiku wa leo? Vema, afadhali—afadhali uwe tayari. Nami nitaanza, nitaongoza nyimbo na kadhalika tunapoendelea basi. Wakati wakininii … [Ndugu Neville anasema, "Kuna nguo zozote nyuma hapa, Doc?" — Mh.] Nguo za ubatizo, Doc, upesi sana. Vema.

Hebu tuimbe mmoja wa hizi ninii nzuri za kale… [Ndugu Branham anaongoza kuimba kwa kusanyiko, wakati Ndugu Neville anambatiza yule dada — Mh.]

[Sehemu tupu kwenye kanda — Mh.] Na mpaka tutakapofanya jambo hilo, tunapoondoka, hatuna budi kufanya nini?

Peleka Jina la Yesu,
Naanguka kifudifudi miguuni Pake,
Mbinguni tutamvalisha, Taji Yeye, Ndiye Mfalme wa wafalme,
Safari yetu itakapokwisha.

Vema, tusimame kwa miguu yetu!

Peleka Jina la Yesu na wewe,
Mwana wa huzuni shida;
Itakupa furaha na faraja …

Nitawaambieni tufanye nini. Geuka moja kwa moja na kupeana mikono na mtu fulani pale, na kusema, "U hali gani, ndugu? Hakika nina furaha kuwa katika huduma pamoja nanyi."

Jina la thamani, Ee ni tamu iliyoje
… Na furaha ya Mbinguni;
Jina la thamani, Jina la thamani, Ee …

Mahubiri Na
William Marrion Branham
"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7

www.messagehub.info